2026
Januari - Marchi

Gombo la 102, Na.1
MASOMO YA BIBLIA YA SHULE SABATO
Watu Wazima



# Mambo Makuu Kutoka kwa Manabii Wadogo

Jumbe za kale kutoka Mbinguni,
bado zinafaa leo.

# Yaliyomo

**SHULE YA SABATO**


1. Ombi la Upendo wa Hosea ..............................5
2. Wakati wa Hesabu ......................................10
3. Kujitayarisha kwa Tumaini ...........................15
4. Kuthamini Rehema za Mungu ..................20
5. Yoeli: Mtume aliyetakaswa ...........................25
6. Wito wa Amosi kwa kujitayarisha ...................31
7. Nguvu katika Toba .....................................36
8. Tayari Tunajua Tunachopaswa Kufanya! ........41
9. Mabadiliko ya Tabia ....................................46
10. Heshima kwa Mwenye kujua yote ......................52
11. Kukesha Kumtukuza Mungu................................57
12. Matukio ya Wakati wa Mwisho ...................62
13. Ombi la Mwisho la Malaki ...........................67


**Masomo ya Biblia ya shule ya sabato** ni utaratibu wa mafundisho ya kila siku, msingi wake pekee ni juu ya Biblia na Roho ya Unabii pasipo maelezo ya nyongeza. Nukuu itolewe kwa ufupi kadri iwezekanavyo, ili kueleketeza ufahamu. [ ] mabano huwekwa baadhi ya sehemu ili kusaidia kuelewa jambo kwa usahihi. Jifunze zaidi katika chanzo kilichopendekezwa.


Masomo ya shule ya sabato (USPS 005 - 118), Gombo la 102, Toleo No. 1, Januari - Marchi 2026 imechapishwa na Baraza kuu Ulimwenguni (GC) - Seventh Day Adventist Reform Movement, Idara ya shule ya sabato.


Nakala zote©2026, zinachapishwa na kusambazwa na Reformation Herald Publishing Association, 5240 Hollins Road, Roanoke, Virginia 24019 - 5048, U.S.A Virginia 24022-9993. nchini Marekani.



Imetafsiriwa na: **SDA Reform Movement, Tanzania Mission,** Idara ya shule sabato, S.L.P 1342, DODOMA TANZANIA

# Utangulizi

Ingawa tunawaita manabii "wadogo," ujumbe wao si mdogo! Jina hilo linatokana tu na ukweli kwamba vitabu walivyoandika ni vifupi. Bado jumbe hizi zilizojaa nguvu ni za nguvu, za moja kwa moja, na zinafaa sana kwa leo. Hii ndiyo sababu wanafunzi wa shule ya Sabato ulimwenguni kote watazingatia Mambo Muhimu Kutoka kwa Manabii Wadogo kwa muda wa miezi mitatu ijayo kama uwekezaji wa wakati unaofaa katika maandalizi yetu ya kufungwa kwa rehema na kurudi kwa Kristo.

Manabii wadogo hawaleti ujumbe laini na rahisi. La hasha ujumbe wao hukata kama shoka lililowekwa kwenye mzizi wa mti. "Mungu hatumi wajumbe ili kumsifia mdhambi. Hapeleki ujumbe wa amani kumliwaza katika usalama wa hatari ya kifo mtu asiyetakasika. Anaweka mizigo mizito juu ya dhamiri ya mtenda-maovu, na kuichoma roho kwa mishale ya kujiona hatia." — *The Desire of Ages*, p.104.

"Mungu amekuwa mwaminifu siku zote katika kuadhibu uharifu. Aliwatuma manabii kuwaonya wakosefu, kushutumu dhambi zao, na kutamka hukumu dhidi yao. Wale wanao oji ni kwanini Neno la Mungu limeleta dhambi za watu Wake hadharani ili wenye dhihaka wacheke na watakatifu walie, lazima watafakari kuwa yote yaliandikwa kwa ajili ya mafundisho, ili kwamba waepuka maovu yote yaliyonakiliwa hkna kuiga yale ya haki ya wale waliomtumikia Bwana." — *Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 12.

"hata Mwenendo mbaya mmoja wa tabia, shauku moja ya dhambi inayotunzwa, mwishowe itapunguza nguvu yote ya injili. Uchungu wa wajibu na raha za dhambi ni kamba ambazo shetani huwafunga watu katika mitego yake. Wale ambao wangependelea kufa kuliko kutenda kitendo kibaya ndiyo tu watakaopatikana wakiwa waaminifu." — *Ibid.*, vol. 5, p. 53.

Manabii wadogo waliwaita watu wa mungu kuwa macho, kuelewa mpango wa mungu, na kukubali kazi yake mioyoni mwao. Huu ndio ujumbe hasa tunaouhitaji kuusikia pia.

"Ndugu, ambao Kweli za Neno la Mungu zimefunguliwa kwenu, ni sehemu gani mtatenda katika matukio ya mwisho ya historia ya ulimwengu huu? Je, uko macho na Ukweli huu adhimu? Je, mnatambua kazi kuu ya maandalizi inayoendelea mbinguni na duniani? Wale wote walioipokea nuru hiyo, waliopata nafasi ya kuusoma na kuusikia unabii ule, wayatunze yaliyoandikwa humo; „kwa maana wakati umekaribia." Hebu mtu yeyote sasa asicheze na dhambi, chanzo cha kila taabu katika ulimwengu wetu. Usibaki tena katika uchovu na ujinga wa kutojali. Usiruhusu hatima ya roho yako ibaki juu ya kutokuwa na hakika. Jua kuwa uko kikamilifu kwenye Upande wa Bwana." — *Ibid*.,vol.6,pp.404.

Bwana na atuongoze tunapojifunza masomo haya!

*Idara ya shule ya sabato GC*

# Sadaka za Sabato ya Kwanza

Sabato, Januari 3, 2026

**Makao Makuu huko Siguatepeque, Honduras**



Honduras ni nchi ya pili kwa ukubwa katika Amerika ya Kati. Katika eneo lenye ukubwa wa maili za mraba 43,433 ($km^2$ 112,492), iko katikati na inapakana na mataifa ya Guatemala, El Salvador, na Nikaragua, kusini na Bahari ya Pasifiki kwenye Ghuba ya Fonseca, na kaskazini na Ghuba ya Honduras, mlango mkubwa wa Bahari ya Karibea. Kati ya wakaaji milioni 10.8, 48.7% ni Wakatoliki, 41% Waprotestanti, 8% wasioamini kwamba kuna Mungu, au wanaodai kutokuwa na dini, na 3% ni wa dini zingine. Lugha rasmi ni Kihispania; mauzo ya nje ya kitaifa kimsingi ni ya kilimo, ikifuatiwa na vifaa vya kielektroniki.

SDARM ilifika katika miaka ya 1960 kwa ziara ya ndugu zetu Silvestre Cabanillas kutoka Perú na Felipe García kutoka Argentina. Baada ya miaka mingi ya kazi, ujumbe ulienea hadi kufikia mwaka wa 2016, Muungano wa Honduras ulipangwa, ukijumuisha Nyanja tatu zenye washiriki 542 na takriban wageni 700 wa kawaida wanaohudhuria mara kwa mara.

Kwa sababu ya umri wa baadhi ya majengo ya makao makuu ya field na union, yameharibika kwa miaka mingi. Baadhi yao bado hayajakamilika,na mojawapo ya Nyanja zetu haina makao makuu ya utawala. Tumefanya jitihada kubwa kuandaa nafasi zinazofaa kwa ajili ya ofisi zetu, vyumba vya mikutano kwa ajili ya makongamano, na uendeshaji wa shule yetu ya mishonari kwa ajili ya kazi inayoongezeka. Hii ndiyo sababu tunaomba ukarimu wenu, ili kwa pamoja tuweze kufikia ndoto yetu ya kuwa na makao makuu ambayo yanafanya kazi kama vinara vya ukweli, ambapo wengi wanaweza kuja kumjua Yesu kwa shukrani.

Bwana hutuchochea tushirikiane wakati wa kutekeleza miradi ya kazi Yake, iliyoonyeshwa katika mwongozo Wake kwa Musa: "waambiewana wa Israeli kwamba wanitwalie sadaka; Kutoka 25:2.Ujitoaji kwa Mungu na roho ya dhabihu vilikuwa matakwa ya kwanza ya kujenga makao ya Aliye Juu Zaidi. Jumuiya nzima ilijibu kwa kauli moja: "Wakaja, kila mtu ambaye moyo wake ulimhimiza, na kila mtu ambaye roho yake ilimfanya kuwa apenda, nao wakaleta sdaka za kumpa Bwana, kwa kazi ya hema ya kukutania" (Kutoka 35:21).

Tunakushukuru mapema kwa usaidizi wako wa ukarimu katika mradi huu. Mungu akubariki sana.

*Ndugu na dada zenu kutoka Honduras*

SABATO, JANUARI 3, 2026

Somo la 1

# Ombi la Upendo wa Hosea

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Nami nitakuposa kwa uaminifu, nawe utamjua Bwana" (Hosea 2:20).

**Inapendekezwa kusoma**:*Testimonies for the Church*, vol.6, pp.404–410.

"Sasa, wakati sauti tamu ya rehema ingali inasikika, wakati bado haujachelewa sana kwa makosa kurekebishwa, wakati mnapoitwa leo, ikiwa mtaisikia sauti yake, msifanye mioyo yenu kuwa migumu."— *Counsels on Stewardship*, p.99.

## 1. WITO MGUMU WA KUAMKA

Jpil, Dis 28

a. Eleza maisha magumu ya manabii wa Mungu. Yakobo 5:10.

---

"Wale ambao Mungu amewakabidhi majukumu muhimu hawakulelewa katika raha na anasa; manabii wakuu, viongozi na waamuzi wa uteuzi wa Mungu, wamekuwa watu ambao tabia zao ziliundwa na hali halisi ya maisha." — *The Signs of the Times*, February 19,1880.

b. Ni jinsi gani Mungu alionyesha kwa Hosea uhusiano kati yake na watu Wake wasio waaminifu? Hosea 1:1–9; Yeremia 3:14; (linganisha 2 Wakorintho 11:2).

---

"Katika Biblia tabia takatifu na ya muda wote ya uhusiano kati ya Kristo na kanisa lake inawakilishwa na muungano wa ndoa. Bwana amewaunganisha watu wake na yeye mwenyewe kwa agano thabiti, yeye akiahidi kuwa Mungu wao, na wao wakiahidi kuwa watu wake na wake yeye peke yake.. . . .

"Kutokuwa mwaminifu kwa kanisa dhidi ya Kristo kwa kuruhusu ujasiri na mapenzi yake kugeuziwa mbali na Kristo, na kuruhusu moyo wake kujazwa na mambo yanayohusiana na kuyapenda mambo ya dunia, kunafananishwa na kuvunja kiapo cha ndoa. Dhambi ya Israeli ya kumwacha Bwana inawakilishwa kwa mfano huu;." — *The Great Controversy*, p. 381.

a. **Baada ya kutangaza hukumu, ni ahadi gani ya matumaini ambayo Mungu aliwapa Israeli? Hosea 1:10.**

---

"Mungu anaweza kwa wingi kubadilisha mioyo ya Myahudi na Myunani sawa, na kumpa kila muumini katika Kristo baraka zilizoahidiwa kwa Israeli. 'Na kama Isaya alisema hapo awali, kama Bwana wa Sabato asingalituachia uzao, tungekuwa kama Sodoma, tungekuwa kama Gomora.'. . .

"Ijapokuwa adhabu ya kutisha iliyotangazwa juu ya Wayahudi kama taifa wakati wa kumkataa Yesu wa Nazareti, wameishi kutoka kizazi hadi kizazi wanaume na wanawake wengi wa vyeo, wanaomcha Mungu ambao wameteseka kimya kimya. Mungu ameifariji mioyo yao katika dhiki na ameona kwa huruma hali yao ya kutisha. Amesikia maombi ya uchungu ya wale ambao wamemtafuta kwa moyo wote kwa ufahamu sahihi wa neno lake.Wengine wamejifunza kuona katika Mnazareti wa hali ya chini ambaye mababu zao walimkataa na kumsulubisha, Masihi wa kweli wa Israeli. Kwa vile akili zao zimefahamu umuhimu wa unabii uliozoeleka kwa muda mrefu sana ambao umefichwa na mapokeo na tafsiri potofu, mioyo yao imejawa na shukrani kwa Mungu kwa zawadi isiyoneneka ambayo Yeye humkabidhi kila mwanadamu anayechagua kumpokea Kristo kama Mwokozi wa kibinafsi." — *The Acts of the Apostles*, p.379.

b. **Mtume Paulo anarudiaje ukweli huu wenye kufariji? Warumi 9:25–27.**

---

"Injili hii itakapowasilishwa kwa utimilifu wake kwa Wayahudi, wengi watamkubali Kristo kama Masihi. Miongoni mwa wahudumu Wakristo kuna wachache tu wanaohisi wameitwa kufanya kazi kwa ajili ya watu wa Kiyahudi; lakini kwa wale ambao wamepitishwa mara kwa mara, pamoja na wengine wote, ujumbe wa rehema na matumaini katika Kristo utakuja.

"Katika utangazaji wa mwisho wa injili, wakati kazi maalum itafanywa kwa ajili ya tabaka za watu waliopuuzwa hadi sasa, Mungu anatarajia wajumbe Wake wapendezwe hasa na Wayahudi wanaowapata katika sehemu zote za dunia. . . .

"Miongoni mwa Wayahudi kuna wengine ambao, kama Sauli wa Tarso, ni hodari katika Maandiko, na hao watatangaza kwa nguvu za ajabu kutoweza kubadilika kwa sheria ya Mungu. Mungu wa Israeli atatimiza hili katika siku zetu. Mkono wake haukufupishwa hata usiweze kuokoa. Watumishi Wake wanavyofanya kazi kwa imani kwa ajili ya wale ambao wamepuuzwa na kudharauliwa kwa muda mrefu, wokovu Wake utafichuliwa."— *Ibid.*, uk. 380, 381.

## 3. KWA WAPOTOFU NA WAOVU

Jnne, Dis 30

**a. Licha ya uharibifu mkubwa wa kiroho wa watu Wake, ni maombi gani ya upole ambayo Mungu hutoa kwao? Hosea 2:14.**

---

---

"Ni Kweli sasa kama vile Kristo alipokuwa duniani, kwamba kila hatua inayofanywa na injili juu ya utawala wa adui inakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa majeshi yake makubwa. Mzozo ambao upo juu yetu sasa utakuwa mbaya zaidi kuwahi kushuhudiwa. Lakini ingawa Shetani anawakilishwa kuwa na nguvu kama yule mtu mwenye nguvu aliyejihami, uharibifu wake utakuwa kamili, na kila mtu anayeungana naye katika kuchagua uasi badala ya uaminifu ataangamia pamoja naye.

"Roho wa Mungu azuiaye hata sasa anaondolewa katika ulimwengu. Vimbunga, dhoruba, tufani, moto na mafuriko, majanga ya baharini na nchi kavu, hufuatana kwa haraka. Sayansi inatafuta kueleza haya yote. Ishara zinazozidi kutuzunguka, zikieleza juu ya ukaribu wa Mwana wa Mungu, zinahusishwa na kitu kingine chochote isipokuwa sababu ya Kweli. Watu hawawezi kutambua malaika walinzi wanaozuia pepo nne ambazo hazitavuma hadi watumishi wa Mungu wawe wametiwa muhuri; lakini Mungu atakapo waamuru malaika Wake wazifungue pepo, kutakuwa na tukio la ugomvi ambalo hakuna kalamu inayoweza kufikiria. . . .

"Je, pazia lingeweza kuviringishwa nyuma, ungeweza kutambua makusudi ya Mungu na hukumu zinazokaribia kuuangukia ulimwengu uliohukumiwa, ungeweza kuona mtazamo wako mwenyewe, ungeogopa na kutetemeka kwa ajili ya nafsi yako na za wenzako. Maombi ya dhati ya uchungu unaovunja moyo yangeenda mbinguni. Ungelia kati ya ukumbi na madhabahu, ukikiri upofu wako wa kiroho na kurudi nyuma." — *Testimonies for the Church*, vol.6, pp.407,408.

**b. Je, Mungu wetu wa kustaajabisha anawezaje kutoa mwanzo mpya, akitoa tumaini zaidi ya urithi wa dhambi? Hosea 2:15; Zaburi 130:7, 8 .**

---

"Mungu akurehemu. Kwa nini wale ambao wameshikwa na uhalifu hawatadhihirisha toba inayolingana na ukubwa wa uhalifu wao, na kukimbilia kwa Kristo ili kupata rehema, na kuponya, kadiri inavyowezekana, majeraha ambayo wamefanya?" — *The Review and Herald*, Machi 24, 1868.

"Haijalishi mwenye dhambi ni dhaifu kiasi gani; haijalishi makosa yake yalikuwa mengi kiasi gani, Mwokozi atamkubali. Kristo anapenda kila mshiriki wa jamii ya wanadamu; kwa maana amevinunua vyote kwa bei;— na ni bei iliyoje!" — *Ibid.*, Septemba 3, 1903.

## 4. UAMSHO WA KUWAFIKIA WENGINE — Jtan, Dis 31

**a. Eleza uhusiano wa ndani zaidi wa ujitoaji ambao nafsi itakuwa nayo pamoja na Mungu wanapotubu kikweli na kuacha njia zao za dhambi. Hosea 2:16, 17 .**

---

---

" 'Na itakuwa katika siku hiyo, asema Bwana, utaniita Ishi ['Mume wangu,']; wala hutaniita tena Baali ['Bwana wangu,']. Kwa maana nitayaondoa majina ya Mabaali kinywani mwake, wala hawatatajwa tena kwa majina yao.' Hosea 2:14–17." — *Prophets and Kings*, ukurasa wa 298, 299.

**b. Unabii huu wa urejesho wa kiroho utatimizwaje katika siku zetu? Hosea 2:18–20.**

---

"Katika siku za mwisho za historia ya dunia hii, agano la Mungu na watu Wake wanaoshika amri litafanywa upya." — *Ibid.*, p. 299.

"Huku rehema ikidumu, Mwokozi anapofanya maombezi, na tufanye kazi kamili kwa umilele."—*Testimonies for the Church,*vol.6,p.405.

**c. Ni nini msingi wa kuwa watu wa Mungu leo, kulingana na Hosea na Yohana? Hosea 2:23; Yohana 1:12.**

---

"Watembelee majirani zako na uoneshe una nia na wokovu wa roho zao. Amsha kila nguvu ya kiroho iwe katika utendaji. Waambie wale unaowatembelea kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia.Bwana Yesu Kristo atafungua milango ya mioyo yao na atafanya ndani ya nia za mvuto wa kudumu.

"Jitahidi kuwaamsha wanaume na wanawake kutoka katika kupoa kwao kiroho. Waambie jinsi ulivyompokea Yesu na jinsi ulivyobarikiwa tangu upate uzoefu katika huduma Yake. Waambie ni baraka gani huja kwako kadri unavyoketi miguuni pa Yesu na kujifunza masomo ya thamani kutoka katika Neno Lake. Waambie juu ya furaha na shangwe iliyopo katika maisha ya Kikristo. Maneno yako ya uchangamfu, yenye bidii yatawasadikisha kwamba umeipata lulu ya thamani kubwa. Hebu maneno yako ya uchangamfu na yenye kutia moyo yaoneshe kwamba hakika umeipata njia iliyo ya juu. Hii ni kazi ya Kweli ya umishionari, na kadri inavyofanywa, wengi wataamka kama watokao katika ndoto." — *Ibid.*, vol. 9, p. 38.

## 5. MATUNDA YA IMANI

Alh, Jan 1

a. Eleza tokeo tukufu litakalotokea hivi karibuni kati ya wale wanaotii kwa moyo wote ombi la mwisho la Mungu. Hosea 3:4, 5 .

---

---

"Kwa yale makabila kumi, yaliyoasi na kutotubu kwa muda mrefu, hayakupewa ahadi ya kurejeshwa kamili kwa mamlaka yao ya zamani huko Palestina. Mpaka mwisho wa wakati, walipaswa kuwa 'watangatanga kati ya mataifa.' Lakini kupitia Hosea ulipewa unabii ulioweka mbele yao pendeleo la kuwa na sehemu katika urejesho wa mwisho ambao utafanywa kwa watu wa Mungu mwishoni mwa historia ya dunia, wakati Kristo atakapotokea akiwa Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.... [Hosea 3:4, 5 ilinukuliwa.]

"Kwa lugha ya mfano Hosea aliweka mbele ya yale makabila kumi mpango wa Mungu wa kurejesha kwa kila nafsi iliyotubu ambayo ingeungana na kanisa Lake duniani, baraka zilizotolewa na Israeli katika siku za uaminifu wao Kwake katika Nchi ya Ahadi." — *Prophets and Kings,* p. 298.

"'Siku hiyo' 'mabaki wa Israeli, na wale waliopona wa nyumba ya Yakobo, . . .watamtegemea Bwana, Mtakatifu wa Israeli, kwa kweli.' Isaya 10:20 . Kutoka 'kila taifa na kabila na lugha na jamaa' kutakuwako wengine watakaoitikia kwa furaha ujumbe huu, 'Mcheni Mungu, na kumtukuza; kwa maana saa ya hukumu yake imekuja.'Watageuka kutoka katika kila sanamu inayowafunga duniani, na 'watamsujudia Yeye aliyezifanya mbingu, na nchi, na bahari, na chemchemi za maji.' Watajiweka huru wenyewe kutokana na kila mtego na watasimama mbele ya ulimwengu kuwa ukumbusho wa rehema ya Mungu. Wakitii matakwa ya kimungu, watatambuliwa na malaika na wanadamu kuwa wale ambao wamezishika 'amri za Mungu, na imani ya Yesu.' Ufunuo 14:6, 7, 12 ."— *Ibid.*, ukurasa wa 299, 300 .

## MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI

Ijum, Jan 2

1. Je, Mungu anaonyeshaje uchungu anaopata kutokana na upotovu wetu?
2. Ni ujumbe gani katika Hosea unaofunua ustahimilivu mkubwa wa Mungu?
3. Mungu huwatendeaje wale waliomtenda dhambi?
4. Ni nini kinachoweza kuwa matokeo ninapowafikia watu ambao matunda yao yanaonyesha waziwazi kwamba wako mbali na Mungu?
5. Maisha yangu yanawezaje kuwa ukumbusho wa rehema ya Mungu?

SABATO, JANUARI 10, 2026

**Somo la 2**

# Wakati wa Hesabu

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa" (Hosea 4:6, sehemu ya kwanza).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church*,vol.2,pp.604–609.

"Katika kila enzi, uvunjaji wa sheria ya Mungu umefuatwa na matokeo yale yale." — *Prophets and Kings*, p. 297.

## 1. KUNDI LA UPOTOFU

Jpil, Jan 4

a. **Ingawa Mungu amekuwa na ujumbe wa rehema kwa muda mrefu, ni nini kingine Alichomwamuru Hosea atangaze—kitumike zaidi ya mara moja katika historia ya wanadamu? Hosea 4:1.**

---

---

"Wakati watu wa Israeli, katika ibada yao ya Baali na Ashtorethi, walipotoa heshima kuu kwa nguvu za asili, walikata uhusiano wao na yale yote ya kuinua na kutukuza, na wakawa waathirika wa urahisi wa majaribu." — *Prophets and Kings*, p. 281.

"Lakini „mchana huu wa upapa ulikuwa ni usiku wa manane kwa ulimwengu.'".'—J. A. Wylie, The History of Protestantism,b.1,ch.4.Maandiko Matakatifu yalikuwa kwa kiasi kikubwa hayajulikani, si kwa watu tu, bali pia hata kwa makasisi. Kama ilivyokuwa kwa Mafarisayo wa zamani, viongozi wa upapa waliichukia nuru ambayo ingefunua dhambi zao. Sheria ya Mungu, kipimo cha haki, ikiwa imeondolewa, walitekeleza mamlaka yao pasipo mipaka. Ubadhilifu, tamaa ya mali na ufisadi vilishamiri. Watu walijizuia kutokana na uharifu ambao si kwamba ulikuwa wa kuwaletea mali au nafasi nzuri. Majumba ya kitawala ya mapapa na mapadri yalijazwa na matukio ya uovu. Baadhi ya makasisi walifanya hatia kubwa ya uharifu kiasi kwamba watawala wa dunia waliona hali hiyo haivumiliki. Kwa karne kadhaa Ulaya haikufanya maendeleo yoyote katika elimu, sanaa au ustaarabu. Kupooza kwa kimaadili na kielimu kulikuwa kumeiangukia.

"Hali ya ulimwengu chini ya utawala wa Kirumi ilitimiza kwa namna ya kuogofya na kutisha maneno ya nabii Hosea: [Hosea 4:6, 1, 2 alinukuliwa]. Haya yalikuwa matokeo ya kuondoa neno la Mungu." — *The Great Controversy*, p.60.

## 2. KAMA SIKU ZA NUHU

jtat, Jan 5

a. Ujumbe wenye kutisha wa Hosea ulitajaje dhambi hususa ambazo Mungu anachukia—na hilo linarudiwaje hadi siku zetu? Hosea 4:2; Luka 17:26, 27 .

"Uovu katika Israeli wakati wa nusu karne iliyopita kabla ya utekwa wa Waashuri ulikuwa kama ule wa siku za Nuhu, na wa kila zama nyingine ambapo watu wamemkataa Mungu na kujitoa wenyewe kabisa kufanya maovu. Kuinuliwa kwa maumbile juu ya Mungu wa maumbile, kuabudu kiumbe badala ya Muumba, daima kumesababisha uovu mbaya zaidi....Ulinzi wa nafsi ukiwa umevunjwa, waabudu waliopotoka hawakuwa na kizuizi dhidi ya dhambi na walijitoa wenyewe kwa tamaa mbaya za moyo wa mwanadamu." — *Prophets and Kings*, ukurasa wa 281, 282.

"Kwa uwazi kabisa Kristo aliona jinsi hali ya jamii itakavyokuwa katika siku zijazo. Aliona kujitosheleza kutawatawala wanaume na wanawake. Vipi kuhusu uhusiano wa ndoa leo? Je! haijapotoka na kunajisi, kufanywa kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu? Talaka baada ya talaka imeandikwa katika karatasi za kila siku. Hii ndiyo ndoa ambayo Kristo anazungumza juu yake anaposema kwamba kabla ya gharika walikuwa 'wanaoa na kuolewa.' " — *Manuscript Releases*, vol. 7, p. 56.

"Dhambi hii yenyewe, uasherati, ilienea miongoni mwa Israeli ya kale, ambayo ilileta wonyesho wa ishara ya kukasirika kwa Mungu. Hukumu za Mungu zilifuata kwa karibu juu ya dhambi yao mbaya. Maelfu yao walianguka, na miili yao iliyochafuliwa ikaachwa nyikani." — *A Solemn Appeal,* p. 142.

b. Taja baadhi ya matokeo machungu yanayotokana na uasi—na baraka nyingi zinazopatikana kwa kujitiisha chini ya mapenzi ya Mungu. Hosea 4:3–5; Yohana 17:3.

"Bwana aliwapa watu Wake amri, ili kwamba kwa kuzitii waweze kuhifadhi afya yao ya kimwili, kiakili, na kiadili. Walipaswa kuishi kwa utii; lakini kifo ni matokeo ya hakika ya uasi wa sheria ya Mungu."— *Fundamentals of Christian Education*, p. 413.

"Yeye anayechagua njia ya kutotii sheria ya Mungu anaamua hatima yake ya wakati ujao; anapanda kwa ajili ya mwili, akivuna mshahara wa dhambi, hata uharibifu wa milele, kinyume cha uzima wa milele. Kujitiisha kwa Mungu na utii kwa sheria yake takatifu huleta matokeo ya hakika. 'Uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.' "— *Ibid*., p.376.

## 3. KUTHAMINI ROHO WA MUNGU — Jnne, Jan 6

a. Kwa nini ni muhimu sana kwa kila mmoja wetu kuchukua uangalifu wa dhati kwa kila miale ya nuru inayotolewa kwetu kwa neema? Hosea 4:6.

---

---

"Maneno ya Mungu kwa Israeli ya kale yana onyo zito kwa kanisa na viongozi wake leo. Kuhusu Israeli Bwana alisema, 'Nijapomwandikia sheria yangu; lakini walihesabiwa kuwa ni kitu kigeni.' Hosea 8:12 . Na kwa makuhani na walimu alitangaza, 'Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe; . . . kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako.' Hosea 4:6.

"Je, maonyo kutoka kwa Mungu yatapitishwa bila kusikilizwa? Je, nafasi za huduma hazitaboreshwa? Je! dharau ya ulimwengu, kiburi cha akili, kupatana na mila na desturi za wanadamu, vitawazuia wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wasimtumikie Yeye? Je, watalikataa neno la Mungu kama viongozi wa Kiyahudi walivyomkataa Kristo? Matokeo ya dhambi ya Israeli yako mbele yetu. Je, kanisa la leo litachukua onyo?"—*Christ's Object Lessons*, p. 306.

b. Eleza hatari ya kumkataa Roho Mtakatifu. Mathayo 12:31, 32 .

---

"Ni hatari kubwa kutamka neno ulilo na mashaka nalo, hatari ya kuhoji na kukosoa nuru ya kimbingu. Mazoea ya kupinga pasipo uangalifu na heshima huathiri tabia, na huelekeza katika utovu wa heshima na kutoamini. Watu wengi wanaokuwa na mazoea haya wameendelea hivyo pasipo kutambua hatari iliyopo, mpaka walipokuwa katika hali ya kupinga na kukataa kazi ya Roho Mtakatifu." — *The Desire of Ages*, p. 323.

"Ni kwa njia ya Roho Wake ambapo Mungu hufanya kazi juu ya moyo wa mwanadamu; na watu wanapomkataa Roho kwa makusudi na kutangaza kuwa ametoka kwa Shetani, wanakata njia ambayo kwayo Mungu anaweza kuwasiliana nao. Kwa kukataa uthibitisho ambao Mungu amependezwa kuwapa, wanaifungia nje nuru iliyokuwa ikiwaka mioyoni mwao, na matokeo yake wanaachwa gizani... Kwa muda, watu ambao wametenda dhambi hii wanaweza kuonekana kuwa watoto wa Mungu; lakini hali zinapotokea ili kukuza tabia na kuonesha ni roho ya namna gani waliyo nayo, wataonekana kuwa kwenye uwanja wa adui, wakiwa wamesimama chini ya bendera yake nyeusi.

"Ndugu yangu, Roho anakualika leo. Njoo kwa Yesu kwa moyo wako wote. Tubu dhambi zako, ungama kwa Mungu, acha maovu yote, ndipo waweza kujipatia ahadi Zake zote. "Niangalieni Mimi, nanyi mpate kuokolewa," ni mwaliko Wake wa neema." — *Testimonies for the Church*, vol.5, p.634.

# 4. WITO KWA WALIONYUMA

Jtan, Jan 7

**a. Ni jinsi gani Mungu mara nyingi ameeleza hali ya wengi wanaodai kuwa wafuasi Wake—pamoja leo? Hosea 4:7–11, 16**

---

---

"Watu wa Mungu hawako tayari kwa matukio ya kutisha na yanayojaribu mbele yetu, hawako tayari kusimama safi kutoka kwenye uovu na tamaa katikati ya hatari na uharibifu wa enzi hii mbaya. Hawana silaha za haki, na hawajajiandaa kupigana na uovu ulioshamiri. Wengi hawatii amriza Mungu, lakini wanakiri kufanya hivyo. Ikiwa wangekuwa waaminifu kutii amri zote za Mungu wangekuwa na nguvu ambayo ingeleta kuuamini kwenye mioyo ya wasioamini."—*Testimonies for the Church*,vol.2, pp.446,447.

"Wale wanaodai utauwa, lakini hawajatakaswa na Ukweli ambao wanakiri, ila hawatabadilisha mwenendo wao wa vitendo, ambao wanajua ni wa kuchukiza mbele za Mungu, kwa sababu hawajakabiliwa na jaribio la kukemewa mmoja mmoja kwa dhambi zao. Ila Wanaona, kwa shuhuda za wengine, basi kesi yao wenyewe imesondwa kwa uaminifu mbele yao. Wanathamini uovu ule ule. Kwa kuendelea na mwenendo wao wa dhambi, wanakiuka dhamiri zao, wakifanya mioyo yao kuwa migumu, na kuzifanya shingo zao kuwa ngumu, sawa tu na na wale ambao shuhuda ilikuwa umetolewa kwao moja kwa moja. Katika kupitia hizo na kisha wakatae kuacha dhambi zao na kurekebisha makosa yao kwa ungamo la unyenyekevu, toba, na kujidhadhalisha, wanachagua njia yao wenyewe, na wamepewa matokeo sawa, na mwishowe wanaongozwa kuwa mateka na Shetani kutenda mapenzi yake. Wanaweza kuwa na ujasiri kwa sababu wanaweza kuficha dhambi zao wengine wasizijuie na kwa sababu hukumu za Mungu haziji kwa njia inayoonekana juu yao.Wanaweza kuwa na mafanikio katika ulimwengu huu. Wanaweza kuwadanganya wanadamu maskini, wasioweza kuona vizuri na wakachukuliwa kama mifano ya uchaji Mungu wakati wako katika dhambi zao. Lakini Mungu hawezi kudanganywa." — *Ibid.*, pp. 447, 448.

**b. Elezea shauku ya moyo wa Mungu juu ya hali hii. Yeremia 3:14, 15 .**

---

"kutokuziamini shuhuda kumeongezeka kwa kasi kadri watu wanapomwacha Mungu. Na hili lipo katika nyadhifa zote, katika Nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua kile ambacho makanisa yetu yanapaswa kukipitia. Niliona kuwa kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa mbingu, lakini hakuna mtu anayeweza kusema kwamba hili litaendelea hadi lini. Hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa Mungu kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, kama nyota katika usiku wenye dhoruba, huangaza hapa na pale kati ya mawingu." — *Ibid.,* vol. 5, p. 76.

## 5. KIPAUMBELE CHA HARAKA ZAIDI — Alh, Jan 8

**a. Je, mtu anawezaje kuepuka hukumu mbaya zaidi inayoweza kumpata aliyerudi nyuma? Hosea 4:17.**

"Ikiwa kuna hata Mwenendo mbaya mmoja wa tabia, shauku moja ya dhambi inayotunzwa, mwishowe itapunguza nguvu yote ya injili. Kila kujifurahisha kwa shauku hiyo kunaimarisha chuki ya nafsi kwa Mungu. Uchungu wa wajibu na raha za dhambi ni kamba ambazo shetani huwafunga watu katika mitego yake. Wale ambao wangependelea kufa kuliko kutenda kitendo kibaya ndiyo tu watakaopatikana wakiwa waaminifu."— *Testimonies for the Church*, vol.5, p.53.

"Mungu huwaongoza watu wake, hatua kwa hatua. Anawaleta kwenye alama tofauti zilizohesabiwa kudhihirisha kile kilicho moyoni. Wengine huvumilia wakati mmoja, lakini huanguka kwenye hatua inayofuata. Katika kila hatua ya juu moyo hujaribiwa na kupimwa kwa karibu zaidi. Ikiwa watu wanaojiita wa Mungu wataona mioyo yao ikipinga kazi hii ya moja kwa moja, hilo lapaswa kuwaaminisha kuwa wana kazi ya kufanya ili kushinda, ikiwa hawatatapikwa kutoka kinywani mwa Bwana. Malaika alisema: "Mungu ataleta kazi yake karibu na karibu zaidi ili kumjaribu na kumpima kila mmoja wa watu wake." Wengine wako tayari kupokea nukta moja; lakini Mungu anapowaleta kwenye hatua nyingine ya kupimwa, hupungua na kusimama nyuma, kwa sababu wanaona hali hiyo inagonga sanamu moja kwa moja. Hapa wana nafasi ya kuona kile kilicho mioyoni mwao kinachomzuia Yesu. Wanathamini jambo fulani kwa kiwango cha juu zaidi kuliko wanavyothamini ukweli, na mioyo yao haijawa tayari kumpokea Yesu. Watu hujaribiwa na kupimwa kwa muda mrefu kuona ikiwa watatoa sanamu zao na kutii ushauri wa Shahidi wa Kweli. Ikiwa yeyote hatasafishwa kwa kuitii kweli, na kushinda ubinafsi wake, kiburi chake, na tamaa mbaya, malaika wa Mungu wana tamko: "Wamejiungamanisha na sanamu, waache," na wanaendelea na kazi yao, wakiwaacha na tabia zao za dhambi bila kushinda, kwa udhibiti wa malaika wabaya. Wale ambao huja kwa kila hatua, na kupita kila mtihani, na kushinda, bila kujali ni kwa gharama gani, wametii ushauri wa Shahidi wa Kweli, na watapokea mvua ya masika, na hivyo kuwa tayari kwa kunyakuliwa." — *Ibid,* vol. 1, p. 187.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI — Ijum, Jan 9

1. **Neno la Mungu linapofukuzwa, kushutumiwa, au kupunguzwa, nini hutokea?**
2. **Je, ahadi ya ndoa ni ya uzito kiasi gani kama inavyofundishwa katika Maandiko?**
3. **Ni nini hutokea tunapokosa kuthamini ujumbe wa kweli ya sasa?**
4. Kwa nini nijifunze Shuhuda kwa ajili ya Kanisa zilizoandikwa kwa mtu mwingine?
5. Kwa nini ni hatari kushikilia hata dhambi moja inayojulikana?

SABATO, JANUARI 17, 2026

Somo la 3

# Kujitayarisha kwa Tumaini

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Njoni, tumrudie Bwana;maana yeye amerarua, na yeye atatuponya; yeye amepiga, na yeye atatufunga jeraha zetu" (Hosea 6:1).

**Inapendekezwa kusoma:** *The Ministry of Healing*, pp.177–182.

"Katika wakati wa kukusanywa, wakati Mungu amenyoosha mkono wake kukusanya watu wake, juhudi za kuueneza ukweli zitatoa matokeo yake yaliyokusudiwa. Wote wanapaswa kuungana na kuwa, na bidii katika kazi." — *Early Writings*, p. 74.

## 1. JUHUDI POTOFU

Jpil, Jan 11

a.Ikiwa matendo yetu yanamsaliti Mungu, ni nini matokeo ya kutisha? Hosea 5:4–7; Isaya 1:11, 15 .

---

"Ikiwa ukweli wa Mungu haujabadilisha tabia zetu kuwa mfano wa Kristo, ujuzi wetu wote juu yake na ukweli ni kama shaba iliayo na upatu uvumao. [Isaya 1:10–20 imenukuliwa.]

"Hebu wote wanaodai kuzishika amri za Mungu, waliangalie vizuri jambo hili, na waone kama hakuna sababu kwa nini hawana zaidi ya kumiminwa kwa Roho Mtakatifu. Ni wangapi wamejinyanyua nafsi zao kwa ubatili! Wanajiona kuwa wametukuka katika upendeleo wa Mungu, lakini wanawapuuza wahitaji, wanaziba masikio yao wasisikie miito ya waliodhulumiwa, na kusema maneno makali, yenye kukata kwa wale wanaohitaji matibabu tofauti kabisa. Hivyo wanamkosea Mungu kila siku kwa ugumu wa mioyo yao....Hebu kila mshiriki wa kanisa auchunguze moyo wake kwa ukaribu, na kuchunguza mwendo wake wa kutenda, ili kuona kama haya yanapatana na roho na kazi ya Yesu; kwa maana kama sivyo, atasema nini atakaposimama mbele ya Hakimu wa dunia yote? . . .

"Kristo amebainisha maslahi yake na yale ya wanadamu wanaoteseka; na huku akiwa amepuuzwa katika nafsi ya wale wanaoteseka, makusanyiko yetu yote, mikutano yetu yote iliyowekwa, mitambo yote ambayo imewekwa kufanya kazi ili kuendeleza kazi ya Mungu, itakuwa na manufaa kidogo. 'Hili mlipaswa kufanya, na lile lingine msiliache.' 'Umepimwa katika mizani, nawe umeonekana kuwa umepunguka.'"— *The Review and Herald*, August 4, 1891.

## 2. TUMAINI KATIKA MGOGORO

Jtat, Jan 12

**a. Ni onyo gani zito ambalo Mungu aliwapa Efaimu na Yuda—na walifanya kosa gani katika hali ngumu? Hosea 5:8–14 .**

---

---

"Miaka ya mwisho ya ufalme mbaya wa Israeli ilitiwa alama ya jeuri na umwagaji damu ambao haujawahi kushuhudiwa hata katika nyakati mbaya zaidi za ugomvi na machafuko chini ya nyumba ya Ahabu. Kwa karne mbili na zaidi watawala wa makabila kumi walikuwa wamepanda upepo; sasa walikuwa wanavuna kimbunga....Wale ambao wangesimama mbele ya mataifa ya dunia kama wahifadhi wa neema ya kimungu, 'wametenda kwa hila juu ya Bwana' na wao kwa wao. Hosea 5:7. . . .

"Baadhi ya viongozi katika Israeli walihisi kwamba wamepoteza umashuhuri na kutamani kwamba hilo lingerudishwa tena. Lakini badala ya kugeuka kutoka kwa mazoea yale ambayo yalileta udhaifu kwa ufalme, waliendelea katika uovu, wakijipendekeza wenyewe kwamba wakati tukio lilipotokea, wangepata mamlaka ya kisiasa waliyotaka kwa kushirikiana na mataifa." — *Prophets and Kings*, ukurasa wa 279, 280.

**b. Katika saa hii ya shida, ni maneno gani ya tumaini na kusihi ambayo Mungu alimwelekeza nabii ayatangaze? Hosea 5:15; 6:1, 2. Hilo linatuhusu jinsi gani sasa hivi?**

---

"Wahalifu walipewa fursa nyingi za kutubu. Katika saa yao ya ukengeufu mkuu na hitaji kuu zaidi, ujumbe wa Mungu kwao ulikuwa wa msamaha na tumaini." — *Ibid.*, p. 283.

"Nawasihi ndugu zetu waamke. Uwezo wa kiroho utadhoofika na kufa ikiwa hautafanyiwa kazi katika kuleta roho kwa Kristo. Ni kisingizio gani kinaweza kutolewa kwa kupuuza kazi kubwa, na kuu ambayo Kristo alitoa maisha Yake kuitimiza?

"Hatuwezi kumudu katika siku chache tulizonazo hapa duniani kutumia muda wetu katika kufanya mambo madogo madogo na kutokufanya kitu. Tunahitaji kunyenyekea nafsi zetu mbele za Mungu, ili kila moyo upate kunywa katika Kweli, na kuiruhusu kufanya maishani matengenezo yatakayoushawishi ulimwengu kwamba hakika huu ndio Ukweli wa Mungu. Hebu maisha yafichwe pamoja na Kristo katika Mungu. Ni pale tu tunapomtafuta Bwana kama watoto wadogo, tunapoacha kutafuta dosari kwa kaka na dada zetu, na kwa wale wanaotafuta kubeba kwa uaminifu majukumu ya kazi, na kutafuta kuifanya mioyo yetu kuwa sawa na Mungu, anaweza kututumia kwa utukufu wa Jina Lake." — *Testimonies for the Church,* vol. 9, pp. 105, 106.

## 3. KUTHAMINI AHADI

Jnne, Jan 12

**a. Je, ni ahadi gani maalum ya Mungu kwa kanisa lake katika siku za mwisho na kwa nini inahitajika? Hosea 6:3.**

“Katika wakati wa mwisho, wakati kazi ya Mungu duniani inapomalizika, juhudi za dhati zinazotolewa na waumini waliojiweka wakfu chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu zinapaswa kuambatana na ishara maalum za upendeleo wa kimungu. Chini ya mfano wa mvua ya kwanza na ya masika, inayonyesha katika nchi za Mashariki wakati wa kupanda na kuvuna, manabii wa Kiebrania walitabiri utoaji wa neema ya kiroho kwa kiwango cha ajabu juu ya kanisa la Mungu. Kumiminiwa kwa Roho katika siku za mitume kulikuwa mwanzo wa mvua ya awali, au ya kwanza, na matokeo yalikuwa ya utukufu. Hadi mwisho wa nyakati uwepo wa Roho ni kukaa na kanisa la kweli.

“Lakini karibu na mwisho wa mavuno ya dunia, zawadi maalum ya neema ya kiroho imeahidiwa kuandaa kanisa kwa ajili ya kuja kwa Mwana wa Adamu. Kumwagwa huku kwa Roho kunafananishwa na kunyesha kwa mvua ya masika; na ni kwa ajili ya nguvu hii iliyoongezwa kwamba Wakristo wanapaswa kutuma maombi yao kwa Bwana wa mavuno ‘wakati wa mvua ya masika.’ — *The Acts of the Apostles*, pp.54,55.

**b. Ni nini kinachotuzuia kupokea baraka hii kwa ukamilifu? Hosea 6:4–6.**

“Pia niliona kuwa wengi hawajui kiasi iwapasavyo kuwa ili waweze kusimama mbele za Mungu bila kuwa na kuhani mkuu katika hekalu la wakati wa taabu. Wale wanaopokea mhuri wa Mungu aliye hai na kulindwa wakati wa taabu lazima waakisi sura ya Yesu kwa ukamilifu

“Niliona kuwa wengi walikuwa wakipuuzia maandalizi muhimu yanayohitajika na huku wakitazamia wakati wa “Kuburudishwa” na “Mvua ya masika” ili kuwafanya wafae kusimama katika siku ya Bwana na kuishi mbele zake. Oh! Namna gani nilivyowaona wengi wakiwa hawana kimbilio wakati wa taabu, walikuwa wamepuuzia maandalizi muhimu; kwa hiyo wasingepokea burudisho yaani mvua ya masika ambayo ingewafanya wafae kuishi mbele za Mungu Mtakatifu. Wale wanaokataa kuchongwa na manabii na kushindwa kusafisha mioyo yao kwa kutii ukweli na kujidhania kuwa wao ni wema zaidi kinyume na hasa walivyo wakati wa mapigo ndipo watakapotambua kuwa walistahili kuchongwa na kujengwa katika unyoofu. Lakini hakutakuwa na muda wa kufanyiwa hilo wala hapatakuwa na mwombezi wa kuwaombea mbele za Baba....[Ufunuo 22:11 ushindi juu ya kila pingamizi juu ya kiburi, ubinafsi, kupenda ulimwengu, na kunukuliwa.] niliona kwamba hakuna yeyote angeweza kushiriki ‘kuburudishwa’ isipokuwa wapate udhibiti wa kila neno na tendo baya.” — *Early Writings*, p. 71.

## 4. IBADA ILIYOPOTOKA

Jtan, Jan 14

a. Je, ukosefu wa utulivu wa wale wanaodai kuwa watu wa Mungu unaonyeshwaje? Hosea 7:2, 7–11, 15 .

b. Ni hali gani katika siku za Hosea zinazolingana na hatari za kiroho katika kanisa la leo? Hosea 8:1–3; Yeremia 23:1.

"Kuna watu wanaojiita kuwa wacha Mungu ambao humchunga mwenye dhambi kwa uasi wao wenyewe. Wanapuuza amri za Mungu, wakichagua mapokeo ya wanadamu, wakiibatilisha sheria ya Mungu, na kuendeleza uasi. Visingizio wanavyotoa ni hafifu na dhaifu na vitaleta uharibifu kwa nafsi zao na roho za wengine. . . .

"Juu ya wale ambao wamechukua juu yao kazi ya wachungaji wa kundi, watapata hukumu nzito zaidi, kwa sababu wamewasilisha kwa watu hadithi badala ya ukweli. Watoto watainuka na kuwalaani wazazi wao. Washiriki wa Kanisa, ambao wameona nuru na kuhukumiwa, lakini ambao wameamini wokovu wa roho zao kwa mtumishi, watajifunza katika siku ya Mungu kwamba hakuna nafsi nyingine inayoweza kulipa fidia kwa ajili ya makosa yao.Kilio cha kutisha kitapazwa, 'Nimepotea, nimepotea milele.' Watu watahisi kana kwamba wangeweza kuwararua vipande-vipande wahudumu ambao wamehubiri uwongo na kushutumu ukweli. Ukweli safi kwa wakati huu unahitaji matengenezo katika maisha, lakini wanajitenga na upendo wa ile kweli, na juu yao inaweza kusemwa, 'Ee Israeli, umejiangamiza mwenyewe.' Bwana anatuma ujumbe kwa watu, 'Weka baragumu kinywani mwako. Atakuja kama tai juu ya nyumba ya Bwana, kwa sababu wamelihalifu agano langu na kuiasi sheria yangu.' " — *The SDA Bible Commentary* [E.G.White Comments], vol.4, p.1157.

c. Ibada ya sanamu na ibada za uongo zilidhoofishaje Israeli—na tokeo lilikuwa nini? Hosea 8:5, 6 .

"Yale makabila kumi ya Israeli sasa yangevuna matunda ya uasi-imani ambao ulikuwa umetokea kwa kusimamishwa kwa madhabahu za kigeni huko Betheli na Dani." — *Prophets and Kings*, p.285.

## 5. NYAKATI ZA HATARI

Alh, Jan 15

a. **Ni somo gani linalofunzwa na kanuni ya kupanda na kuvuna? Hosea 8:7; Wagalatia 6:7, 8 .**

---

---

"Ulimwengu usioamini..... Walidharau na kukanyaga kweli ya neno la Mungu. Walijiingiza kwenye matumizi ya mavazi ya kupindukia, na walitumia maisha yao kwenye furaha na anasa. Walipanda upepo, wakavuna tufani. Katika nyakati za dhiki na kuchanganyikiwa kwa mataifa kutakuwa na wengi ambao hawakujitoa kikamilifu kwa mivuto potofu ya ulimwengu na kazi za shetani, ambao watajinyenyekeza kwa Mungu na kumrejea kwa mioyo yao yote na kupata ukubali na msamaha.

"Miongoni mwa Watunza Sabato ambao hawakuwa tayari kutoa dhabihu lakini ambao wamejitoa kwa mvuto wa ulimwengu, watapaswa kujaribiwa na kuthibitishwa. Hatari za siku za mwisho zi juu yetu na jaribu ambalo hawakulitarajia liko mbele ya vijana. Wanapaswa kuingia kwenye dhiki kuu na mashaka ya kufadhaisha. Uhalisia wa imani yao utapimwa. Wanakiri kutazamia kuja kwa Mwana wa Adam, wakati miongoni mwao wamekuwa mfano mbaya kwa wasio waamimi.. . . .

"Siku ya uchungu unaopasua moyo iko mbele yetu. Nilioneshwa kwamba shuhuda zilizo dhahiri zinapaswa kutolewa, na kwamba wale watakaokuja kwa ajili ya msaada wa Bwana watapokea baraka yake." — *Testimonies for the Church*, vol.1, pp.268–270.

b. **Kwa nini huu ni wakati wa kulipa uangalifu wa karibu zaidi kwa mapenzi ya Mungu? Hosea 8:12.**

---

"Je, maonyo kutoka kwa Mungu yatapitishwa bila kusikilizwa? Je, nafasi za huduma hazitaboreshwa? Je! dharau ya ulimwengu, kiburi cha akili, kupatana na mila na desturi za wanadamu, vitawazuia wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wasimtumikie Yeye? Je, watalikataa neno la Mungu kama viongozi wa Kiyahudi walivyomkataa Kristo? Matokeo ya dhambi ya Israeli yako mbele yetu. Je, kanisa la leo litachukua onyo?"—*Christ's Object Lessons*, p. 306.

## MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI

Ijum, Jan 16

1. Kwa nini ni muhimu kuishi kupatana na nuru yote tuliyo nayo katika siku hizi za mwisho?
2. Kama ilivyokuwa nyakati za kale, ni nini kinachoweza kuwa kinatukengeusha kutoka kwa misheni yetu?
3. Ni ahadi gani ya thamani ya wakati wa mwisho inayoweza kubadilisha maisha yangu—na kwa nini?
4. Ni lini na kwa nini Mungu anakuja kama tai dhidi ya nyumba ya Bwana?
5. Ni katika sehemu gani za maisha ninahitaji kukata uhusiano fulani wenye kudumu na ulimwengu?

SABATO, JANUARI 24, 2026

**Somo la 4**

# Kuthamini Rehema za Mungu

**FUNGU LA KUKARIRI:** “Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako” (Hosea 13:9).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church*, vol.4, pp.186–213.

“Kila mwale wa nuru uliokataliwa, kila onyo lililopuuzwa au kutosikilizwa, kila uvunjaji wa sheria ya Mungu, ni mbegu iliyopandwa na inayotoa mavuno.” — *The Great Controversy*, p.36.

## 1. SIKU ZA KUJILIWA

Jpil, Jan 18

a. Ni onyo gani linalorejea hadi kufungwa kwa rehema? Hosea 9:7.

---

"[Barnaba] alihangaika sana kwamba Marko asiache huduma, kwa kuwa aliona ndani yake sifa za kustahili ambazo zingemfaa kuwa mfanyakazi mwenye manufaa kwa ajili ya Kristo." Baada ya miaka mingi kusali kwake kwa niaba ya Marko kulithawabishwa sana, kwa kuwa kijana huyo alijitoa bila kujibakiza kwa Bwana na kwa kazi ya kutangaza ujumbe wa injili katika maeneo magumu." — *The Acts of the Apostles,* p. 170.

"Muda ni mfupi, na unachopaswa kufanya lazima kifanyike haraka. Azimia kuukomboa wakati. Usiitafute furaha yako mwenyewe. Amka mwenyewe! Shikilia kazi kwa nia mpya ya moyo. Bwana ataifungua njia mbele yako. Fanya kila juhudi uwezavyo kufanya kazi katika njia na safu ya Kristo, kwa upole na unyenyekevu, ukimtegemea Yeye kwa ajili ya nguvu. Elewa kazi ambayo Bwana anakupa kufanya, na, ukimtumaini Mungu, atakuwezeshwa kuendelea kutoka nguvu hadi nguvu, kutoka neema hadi neema. Utawezeshwa kufanya kazi kwa bidii,kwa subira kwa watu wako maadamu mchana ungalipo kwa maana usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi." — *Testimonies for the Church,* vol.9, p.200.

## 4. NGUVU KATIKA TOBA

Jtan, Feb 11

**a. Ili kumtii Mungu, ni nini kinachofunua ujasiri ambao Yona alihitaji sasa? Yona 3:4.**

---

---

"Wakati wa mafanikio yake ya muda Ninawi ilikuwa kitovu cha uhalifu na uovu. Upulizio umelitambulisha kuwa 'jiji la umwagaji damu, . . . aliyejaa uwongo na unyang'anyi.' Kwa lugha ya kitamathali nabii Nahumu alilinganisha Waninawi na simba mkatili, mkali. akauliza, 'Ni nani,' 'uovu wako haukupita juu yake?' Nahumu 3:1, 19 ." — *Prophets and Kings*, p.265.

**b. Eleza jinsi Mungu alibariki kazi ya Yona kwa njia yenye nguvu—na ueleze kwa nini sisi wenyewe tunapaswa kuamka kuona uamuzi uliofanywa na Ninawi. Yona 3:5–10.**

---

""Ingawa Ninawi ilikuwa mbaya, haikuangukia kabisa kwenye uovu. Yeye 'Huwatazama wanadamu wote' (Zaburi 33:13) na 'kuona kila kito cha thamani' (Ayubu 28:10) aliwaona katika mji huo wengi waliokuwa wakitafuta kitu bora na cha juu zaidi, na ambao, wakipewa fursa ya kujifunza kuhusu Mungu aliye hai, wangeacha matendo yao maovu na kumwabudu Yeye." — Ibid.

"Wakati Yona alipotangaza katika mitaa ya Ninawi kwamba katika muda wa siku arobaini mji ule ungeangamizwa kabisa, Bwana alikubali kujinyenyekeza kwa watu wa Ninawi, na kuongeza muda wao kuangaliwa; lakini bado ujumbe ule wa Yona ulitoka kwa Mungu, na Ninawi ulipimwa kulingana na mapenzi ya Mungu." — *The Great Controversy,* p.406.

"Ni nani ajuaye kama wahubiri ambao ni waaminifu, thabiti, na wakweli wanaweza kuwa wa mwisho ambao watatoa injili ya amani kwa makanisa yetu yasiyo na shukrani? Pengine waharibifu tayari wanafanya mazoezi chini ya mkono wa shetani na wanangojea tu kuondoka kwa wabeba viwango kadhaa ili wachukue nafasi zao, na kwa sauti ya nabii wa uwongo wanalia, „Amani, amani," wakati Bwana hajasema kwamba ni amani. Mimi rahisi kulialia (si mlizi), lakini sasa naona macho yangu yamefunikwa machozi; yanaiangukia karatasi yangu ninapoandika. Inaweza kuwa kwamba unabii wote kati yetu utakuwa umekamilika, na sauti ambayo imewahimiza watu haiwezi kuusumbua tena usingizi wao wa mwili.

"Wakati Mungu atakapofanya kazi yake ya ajabu duniani, wakati mikono mitakatifu itakapokuwa haibebi sanduku tena, ole itakuwa juu ya watu. Laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii, yapasayo amani! Oh, watu wetu kama walivyofanya Ninawi, wangetubu kwa nguvu zao zote na kuamini kwa moyo wao wote, ili Mungu aondoe hasira yake kali kutoka kwao." — *Testimonies for the Church*, vol.5, pp.77,78.

## 5. NINAWI YA LEO HII — Alh, Feb 12

a. Udhaifu wa kibinadamu wa Yona ulijidhihirishaje tena? Yona 4:1–3.

“Yona alipojua juu ya kusudi la Mungu la kuuepusha mji huo kwamba, ijapokuwa uovu wake, ulikuwa umeongozwa kutubu katika magunia na majivu, alipaswa kuwa wa kwanza kushangilia kwa sababu ya neema ya ajabu ya Mungu; lakini badala yake aliruhusu akili yake kukaa juu ya uwezekano wa kuonekana kwake kama nabii wa uongo. Akiwa na wivu juu ya sifa yake, alipoteza kuona thamani kubwa zaidi ya nafsi katika jiji hilo la unyonge. . . .

“Kwa mara nyingine tena alikubali mwelekeo wake wa kuhoji na kutilia shaka, na kwa mara nyingine tena alilemewa na kuvunjika moyo.” —*Prophets and Kings*, p.271.

b. Tofauti na Yona, kwa nini tunaweza kushangilia kikweli nafsi zinapotubu? Yona 4:4, 11 .

“Somo ni kwa ajili ya wajumbe wa Mungu leo, wakati majiji ya mataifa yanahitaji kwa hakika ujuzi wa sifa na makusudi ya Mungu wa kweli kama vile Waninawi wa kale walivyohitaji. Mabalozi wa Kristo wanapaswa kuwaelekeza watu kwenye ulimwengu wa hali ya juu, ambao kwa kiasi kikubwa umepotea.” — *Ibid.*, p. 274.

“Wajumbe wa Mungu katika miji mikubwa wasikatishwe tamaa juu ya uovu, udhalimu, upotovu, ambao wanaitwa kukabiliana nao huku wakijitahidi kutangaza habari njema ya wokovu. Bwana angemchangamsha kila mfanyakazi kama huyo kwa ujumbe uleule aliompa mtume Paulo katika Korintho: ‘Usiogope, bali nena, wala usinyamaze;kwa kuwa mimi nipo pamoja nawe, wala hapana mtu atakayekushambulia ili kukudhuru, kwa maana mimi nina watu wengi katika mji huu.’ Mdo. 18:9, 10 .... Katika kila jiji, ingawa limejaa jeuri na uhalifu, kuna wengi ambao kwa mafundisho yanayofaa wanaweza kujifunza kuwa wafuasi wa Yesu.” — *Ibid.*, p. 277.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI — Ijum, Feb 13

1. Kwa nini kutengana kwa njia ya uchujaji ni muhimu?
2. Ni uthibitisho gani katika maisha yangu ambao umefunua kwamba Mungu ndiye anayetawala, sio mimi?
3. Jaribio la Yona linafundisha nini tunaposhawishiwa kufikiri kwamba Mungu hawezi kunisikia?
4. Ingawa Ninawi liliharibiwa baadaye, kwa nini hilo halikutokea katika siku 40?
5. Ninahitaji kukumbuka nini kuhusu nafsi katika miji mibaya iliyo karibu nami?

SABATO, FEBRUARI 21, 2026

**Somo la 8**

# Mpango wa Mungu wa Urejesho

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Enyi watu wangu, nimewatenda nini? nami nimekuchosha kwa habari gani? shuhudieni juu yangu. Kwa maana nalikupandisha kutoka nchi ya Misri, na kukukomboa utoke katika nyumba ya utumwa." ( Mika 6:3, 4 , NW, sehemu ya kwanza).

**Inapendekezwa kusoma:** *The Great Controversy*, pp.253–264.

"Hakuna mzazi wa kidunia aliyewahi kumsihi kwa bidii mtoto anayekosea kama Yeye ambaye alituumba anavyomsihi mkosaji." - *Testimonies for the Church*, vol.8,p. 275.

## 1. MGOGORO KATIKA YUDA

Jpil, Feb 15

a. **Ni mambo ya aina gani yalikuwa yakiendelea katika Yuda wakati Ahazi alipopanda kiti cha ufalme? 2 Wafalme 16:2–4.**

---

"Kutawazwa kwa Ahazi kwenye kiti cha ufalme kulileta Isaya na washirika wake uso kwa uso na hali zenye kuogofya zaidi kuliko zote zilizokuwako wakati huo katika milki ya Yuda. Wengi ambao hapo awali walikuwa wamestahimili uvutano wenye kushawishi wa mazoea ya ibada ya sanamu sasa walikuwa wanashawishiwa kushiriki katika ibada ya miungu ya kipagani.Wakuu katika Israeli hawakuwa waaminifu kwa imani yao; manabii wa uongo walikuwa wakitokea wakiwa na jumbe za kupotosha; hata baadhi ya makuhani walikuwa wakifundisha kwa ajili ya malipo. Hata hivyo, viongozi katika ukengeufu bado walihifadhi aina za ibada ya kimungu na kudai kuwa wamehesabiwa miongoni mwa watu wa Mungu." — *Prophets and Kings*, p.322.

b. **Je, Mungu aliitikiaje machukizo haya? Yeremia 7:30–34.**

---

"Kwa dhana potovu za sifa za kimungu, mataifa ya kipagani yaliongozwa kuamini dhabihu za kibinadamu zilizokuwa muhimu ili kupata kibali cha miungu yao; na ukatili wa kutisha zaidi umefanywa chini ya aina mbalimbali za ibada ya sanamu. Miongoni mwao ilikuwa ni ile desturi ya kuwapitisha watoto wao motoni mbele ya masanamu yao.... Katika nyakati za ukengeufu mkuu machukizo haya yalitawala, kwa kiasi fulani, miongoni mwa Waisraeli."— *Patriarchs and Prophets*, p. 337.

## 2. MAONYO YA LEO

Jtat, Feb 16

a. **Zaidi ya Isaya na Yeremia, ni nani wengine ambao Mungu aliwaita watoe unabii kwa Yuda—na kwa nini? Mika 1:1–5; 2:1, 2, .**

b. **Katika utawala wa Hezekia, mwana wa Ahazi, Mika alipaswa kukabiliana na manabii wa uwongo jinsi gani—na kwa nini hilo pia lahitajiwa leo? Mika 3:5–8; 2 Timotheo 4:3, 4 .**

"Mungu anapopeleka kwa wanadamu maonyo muhimu sana kiasi kwamba yanaonyeshwa kama yanatangazwa na malaika warukao katika mbingu, anataka kila mtu aliyejaaliwa uwezo wa akili kuzingatia ujumbe huo. Hukumu za kuogofya zilizotajwa dhidi ya kumsujudu yule mnyama na sanamu yake (Ufunuo 14:9-11), ingewafanya wote wajifunze kwa bidii unabii huo ili kujua alama ya mnyama ni nini, na ni kwa jinsi gani wanaweza kuepuka kuipokea. Lakini makundi makubwa ya watu yanageuza masikio yao wasisikie ukweli na wanazigeukia hadithi za uongo. Mtume Paulo alisema, akiangalia mbele mnamo siku za mwisho: "Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima." 2 Timotheo 4:3. Wakati huo umefika sawasawa. Watu wengi hawataki ukweli wa Biblia, kwa sababu unaingilia mapenzi ya moyo wa dhambi unaopenda dunia, na mahali pake Shetani anawapatia madanganyo wanayopenda.

"Lakini Mungu atakuwa na watu wake duniani watakaoidumisha Biblia, na Biblia pekee, kama kiwango cha mafundisho yote na msingi wa matengenezo yote. Maoni ya wasomi, mahitimisho ya kisayansi, mafundisho ya makanisa yatokanayo na maamuzi ya mabaraza ya kidini, kwa kadiri yalivyo tofauti na yasivyokubaliana kama yalivyo makanisa yenyewe yanayowakilishwa nayo, au maamuzi ya sauti ya walio wengi – moja kati ya hayo au yote hayo yasiwe ushahidi wa kukubali au kukataa jambo lolote linalohusu imani ya dini. Kabla ya kukubali fundisho lolote au agizo lolote, lazima tudai kupata maneno ya wazi kwamba "Hivi ndivyo asemavyo Bwana." — *The Great Controversy*, pp.594,595.

c. **Eleza hatari ya kujiona kuwa mwadilifu pekee. Mika 3:9–12.**

"[Mika 3:9–11 imenukuliwa.]Kwa uaminifu kabisa, maneno haya yalielezea kuhusu upotofu na kujihesabia haki kwa wakazi wa Yerusalemu. Wakijigamba kwamba wanashika mafundisho ya sheria ya Mungu, walikuwa wakikiuka kanuni zake zote.. . . .wakati walimchinja Mwokozi wao kwa sababu alikemea dhambi zao, hiyo ilikuwa ni kujihesabia haki wao wenyewe kama walivyojiona wenyewe kwamba ni taifa lililopendwa na Mungu na wakimtegemea Bwana awaokoe na adui zao. " — *Ibid.*, p. 27.

## 3. UREJESHO ULIOTABIRIWA

Jnne, Feb 17

a. Ni nini kilichelewesha hukumu iliyotabiriwa na Mika—na hilo linaonyeshaje rehema ya Mungu? Yeremia 26:18, 19 .

b. Ni ahadi gani ambayo Mungu huwapa wale wanaoshinda—na hii inaelekezaje kwenye kurejeshwa kwa Edeni? Mika 4:1, 2, 6–8 .

"Shetani, kwa kufaulu kwake katika kugeuza mwanadamu kando kutoka kwenye njia ya utii, akawa 'mungu wa ulimwengu huu.' 2 Wakorintho 4:4 . Utawala ambao hapo awali ulikuwa wa Adamu ulipitishwa kwa mnyang'anyi. Lakini Mwana wa Mungu alipendekeza kuja duniani ili kulipa adhabu ya dhambi, na hivyo sio tu kumkomboa mwanadamu, bali kurejesha utawala uliopotezwa.Ni juu ya urejesho huu ambapo Mika alitabiri aliposema, 'Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni, utajiliwa naam, mamlaka ya kwanza.' Mika 4:8 ." — *Prophets and Kings*, p. 682.

"Hamu ya kina inayoonekana miongoni mwa wanadamu kuhusu maamuzi ya mahakama za kidunia huwakilisha kwa uhafifu tu shauku inayoonekana katika mahakama za mbinguni wakati majina yaliyoingizwa katika kitabu cha uzima yanapoletwa kupitiwa mbele ya Hakimu wa ulimwengu wote. Mwombezi wetu wa mbinguni anaomba kwamba wale wote walioshinda kwa imani katika damu yake wasamehewe dhambi zao, kwamba wapate kurejeshwa nyumbani kwao Edeni, na kuvikwa taji kama warithi pamoja naye wa ile "mamlaka ya kwanza." Mika 4:8. Shetani katika juhudi yake yote ya kuidanganya na kuijaribu jamii yetu alikuwa amefikiria kuuvuruga mpango wa Mungu wa kumwumba mwanadamu; lakini sasa Kristo anaomba kwamba mpango huu utekelezwe sasa kana kwamba mwanadamu hakupata kuanguka kamwe." — *The Great Controversy,* pp.483,484.

c. Mika na wengine walitabirije ushindi huo wa mwisho? Mika 4:10–12.

"Manabii ambao matukio haya makuu yalifunuliwa walitamani sana kuelewa umuhimu wao. . . .

"Kwetu sisi ambao tunasimama kwenye ukingo wa utimilifu wao, ni wakati gani wa kina, hamu ya maisha iliyoje, haya ni maelezo ya mambo yajayo—matukio ambayo, tangu wazazi wetu wa kwanza walipogeuza hatua zao kutoka Edeni, watoto wa Mungu wamekesha na kungoja, kutamani na kuomba!" — *Education*, p. 183.

## 4. MVUA YA BARAKA KUTOKA MBINGUNI — Jtan, Feb 18

**a. Katika kumiminiwa kwa wingi kwa rehema ya Mungu, unabii wa Mika 5:1, 2 unaofunua hali ya kimungu ya milele ya Kristo ulitimizwa jinsi gani—lakini uzuri wake ulipuuzwa jinsi gani? Mathayo 2:3–6.**

---

"Kupitia wazee na manabii, na pia kupitia vielelezo na mifano , Mungu alizungumza na ulimwengu kuhusu kuja kwa Mkombozi kutoka dhambini. Msururu mrefu wa unabii ulioongozwa na roho ulielekeza kwenye ujio wa 'Tamaa ya mataifa yote.' Hagai 2:7 . Hata mahali pale pale alipozaliwa na wakati wa kutokea kwake vilibainishwa kwa ufupi. Mwana wa Daudi lazima azaliwe katika jiji la Daudi." — *Prophets and Kings*, p. 697.

"Wakati ule wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza makuhani na waandishi wa Mji Mtakatifu, ambao walikabidhiwa mausia ya Mungu, wangeweza kuzitambua dalili za nyakati na kukutangaza kuja kwake Yeye Aliyeahidiwa. Unabii wa Mika ulipataja mahali atakapozaliwa; Danieli alitaja wakati mahsusi wa kuja kwake. Mika 5:2; Danieli 9:25. Mungu alikabidhi unabii huu kwa viongozi wa Kiyahudi; walikuwa hawana udhuru kwa kutokujua na kutowatangazia watu kwamba kuja kwake Masihi kulikuwa kumekaribia. Ujinga wao ulikuwa ni matokeo ya upuuzi katika dhambi. Wayahudi walikuwa wakijenga kumbukumbu za manabii wa Mungu waliouawa, wakati kwa kujiweka chini ya wakuu wa dunia hii walikuwa wanatoa heshima zao kwa watumishi wa Shetani. Wakiwa wamezama katika tamaa zao za kutaka nafasi na mamlaka miongoni mwa wanadamu, walikosa kuona heshima za kimbingu walizokabidhiwa na Mfalme wa mbinguni." — *The Great Controversy*, p.313.

**b. Ni nini kilifunuliwa kama mpango wa Mungu kwa mabaki ya Israeli? Mika 5:7.**

---

"Yule aliye na amani na Mungu na wanadamu wenzake hawezi kuhuzunishwa. Wivu hautakuwamo moyoni mwake; kuwawazia watu mabaya hakutapata nafasi mle; chuki haiwezi kuwamo. Moyo unaopatana na Mungu unashiriki amani itokayo mbinguni, nao utaueneza pande zote mvuto wake uletao furaha kwa wote. Roho ya amani itatua kama umande juu ya mioyo iliyochoka na ile inayosumbuka kutokana na mashindano yaliyomo duniani.

"Wafuasi wake Kristo hutumwa duniani na neno la ujumbe wa amani. Ye yote, ambaye kwa mvuto wake wa kimya asioujua wa maisha matakatifu, atakayeudhihirisha upendo wa Kristo; ye yote ambaye, kwa neno au tendo, atamwongoza mwingine kuiacha dhambi na kuutoa moyo wake kwa Mungu, huyo ndiye msuluhishi.. . . .

"Wema wa Kristo huwazunguka kama manukato. Maisha yao ya kupendeza, na uzuri wa tabia yao, huwadhihirishia walimwengu ya kuwa wao ni wana wa Mungu." — *Thoughts From the Mount of Blessing,* pp. 27-28.

## 5. HAKI YA BWANA

Alh, Feb 19

a. Mika alitoa ombi gani la ajabu wakati wa utawala wa Ahazi, akiwaalika Waisraeli waliokosea warejee kwenye ushikamanifu wao kwa Mungu? Mika 6:2–5.

---

---

"Mungu ana mabishano na wote wanaotenda dhulma ndogo; kwani kwa kufanya hivyo wanakataa mamlaka ya Mungu na kuhatarisha maslahi yao katika upatanisho, ukombozi ambao Kristo ameufanya kwa kila mwana na binti wa Adamu. Je, itafaa kufanya jambo lililo machukizo kwa Mungu?Je! itafaa kuweka juu ya vyetezo vyako moto usio wa kawaida ili kutoa mbele za Mungu, na kusema hakuna tofauti?" — *Testimonies to Ministers*, p. 373.

b. Ni ombi gani la moyoni la watu wengi ambalo Mungu hutamani kujibu? Mika 6:6, 7; Yeremia 8:22; Yohana 1:29.

---

"Haiwezekani sisi, sisi wenyewe, kuepuka shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni mibaya, na hatuwezi kuibadilisha...

"Haitoshi kutambua wema wa upendo wa Mungu, kuona ukarimu, upole wa baba, wa tabia yake. Haitoshi kutambua hekima na haki ya sheria yake, kuona kwamba imejengwa juu ya kanuni ya milele ya upendo. Mtume Paulo aliona haya yote aliposema, 'Naikiri sheria ya kuwa ni njema.''Sheria ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema.' Lakini aliongeza, katika uchungu wa nafsi yake na kukata tamaa, 'Mimi ni mtu wa mwili, nimeuzwa chini ya dhambi.' Warumi 7:16, 12, 14 .Alitamani usafi, uadilifu, ambao ndani yake mwenyewe hakuwa na uwezo wa kuufikia, na akapaza sauti, 'Ewe mtu mnyonge mimi! ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?' Warumi 7:24 , pambizoni.Hiki ndicho kilio ambacho kimepanda kutoka kwenye mioyo yenye mizigo katika ardhi zote na zama zote. Kwa wote, kuna jibu moja tu, 'Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.' Yoh 1:29." — *Stepsto Christ*, pp.18, 19.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI

Ijum, Feb 20

1. Tunapaswa kujua historia gani tunapopanga ibada yetu?
2. Ni nini cha kubainisha mafundisho ya kanisa la Mungu katika siku za mwisho?
3. Kwa nini Mika aliweza kujawa na tumaini la wakati ujao?
4. Eleza tofauti kati ya Wayahudi katika siku ya Kristo na mabaki ya mwisho.
5. Ni nini kinachofanya iwezekane kwa Mungu kufikia mioyo ya watoto Wake wanaokosea?

SABATO, FEBRUARI 28, 2026

**Somo la 9**

# Tayari Tunajua tunachopaswa Kufanya!

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako? ( Mika 6:8 ).

**Inapendekezwa kusoma:** Testimonies for the Church, vol.4, pp.306–313.

"Wale walio na moyo mnyenyekevu, wenye kutumaini, na kupondeka, Mungu hukubali, na husikia maombi yao; na Mungu anapotoa msaada, vikwazo vyote vitashindwa." — *Testimonies for the Church*, vol.4, p.539.

## 1. KWA MTAZAMO WA MUNGU

**Jpil,** Feb 22

a. Nabii Mika aliagizwa kufupisha wajibu wetu kwa Mungu kwa maelezo gani rahisi? Mika 6:8.

"Maneno na sheria ya Mungu, iliyoandikwa katika nafsi, na kuoneshwa katika maisha yaliyowekwa wakfu, matakatifu, vina mvuto wenye nguvu wa kuhukumu ulimwengu. Tamaa, ambayo ni ibada ya sanamu, na husuda, na kupenda dunia, vitang'olewa kutoka katika mioyo ya wale wanaomtii Kristo, na itakuwa furaha yao kutenda haki, kupenda rehema, na kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu. Lo, ni kiasi gani mambo haya yanajumuishwa, kwa kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu! Sheria ya Mungu, ikiwa imeandikwa moyoni, itavuta akili na utashi chini ya utii wa Kristo." — *Testimonies for the Church*, vol.3,p.201.

b. Je, tunakumbushwaje kuhusu uhitaji wa uadilifu ulio bora zaidi? Mika 6:11 .

"Kupotoka kidogo kutoka kwa Ukweli, tofauti kidogo kutoka kwa mahitaji ya Mungu, hufikiriwa kuwa, hata hivyo, siyo dhambi sana vile, wakati faida au hasara ya pesa inapohusika. Lakini dhambi ni dhambi, iwe imetendwa na mwenye mamilioni au ombaomba mitaani. Wale wanaolinda mali kwa uwakilishi wa uwongo wanaleta hukumu juu ya nafsi zao." — *Ibid.,* vol. 4, p. 311.

## 2. HALI YETU DHIDI YA UTUKUFU WA MUNGU — Jtat, Feb 23

a. Ni maelezo gani ya kufaa yanayotolewa kuhusu hali ya wale wanaodai kuwa watu wa Mungu katika siku za Mika? Mika 7:2–4.

“Hakika huu ulikuwa wakati wa hatari kubwa kwa taifa teule. Miaka michache tu, na makabila kumi ya ufalme wa Israeli yangetawanywa kati ya mataifa ya ukafiri. Na katika ufalme wa Yuda pia mtazamo ulikuwa giza. Nguvu za wema zilikuwa zikipungua kwa kasi, nguvu za uovu zikiongezeka.” — *Prophets and Kings*, p.324.

b. Ni mtazamo gani hutusaidia kubaki tukiwa makini kuhusu uhitaji wetu kwa Mungu? Mika 7:5–7; Zaburi 60:11.

c. Eleza tumaini zuri ambalo wote wana pendeleo la kushika kwa imani. Mika 7:8, 9 .

“Mpango wa wokovu wa mbinguni ni mpana vya kutosha kukumbatia ulimwengu wote. Mungu anatamani kumpulizia mwanadamu aliyesujudu pumzi ya uhai. Na hatairuhusu nafsi yoyote kufedheheshwa ambaye ni mkweli katika kutamani kwake kitu cha juu na adhimu kuliko chochote kinachoweza kutolewa na ulimwengu.Daima huwatuma malaika zake kwa wale ambao, huku wakiwa wamezungukwa na mazingira ya kukatisha tamaa zaidi, wanaomba kwa imani wapate mamlaka fulani iliyo juu kuliko wao wenyewe ili kuwamiliki na kuleta ukombozi na amani.Kwa njia mbalimbali Mungu atajifunua kwao na atawaweka wawasiliane na riziki ambazo zitaweka tumaini lao katika Yule ambaye amejitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wote, ‘wamwekee Mungu tumaini lao, wala wasisahau matendo ya Mungu, bali wazishike amri zake.’ Zaburi 78:7 .” — *Prophets and Kings*, pp. 377, 378.

d. Je, Mika anaitukuzaje tabia ya Mungu kwa uwazi? Mika 7:18, 19 .

“Ni ukweli wa ajabu huo!- yeye ni mwenye haki kwa sheria yake mwenyewe, tena ni mwenye kuwahesabia haki wote wamwaminio Yesu. ” — *Thoughts From the Mount of Blessing*, p.116.

## 3. HAKI, REHEMA, UKAMILIFU

Jnne, Feb 24

**a. Je, tunawezaje kufupisha usawa kamili katika tabia ya Mungu? Nahumu 1:3.**

---

---

"Yeye akaaye katika patakatifu pa mbinguni anahukumu kwa haki. Furaha yake ni zaidi kwa watu wake, wakipambana na majaribu katika ulimwengu wa dhambi, kuliko katika jeshi la malaika wanaozunguka kiti chake cha enzi." — *Christ's Object Lessons*, p. 176.

"Uvumilivu wa Mungu ni wa ajabu. Haki hungoja kwa muda mrefu huku rehema ikimsihi mwenye dhambi." — *Ibid*., p. 177.

**b. Katika kutambua kwamba rehema ya Mungu ni muhimu kwa kuwepo kwetu, ni nini kingine tunachohitaji kuendelea kukumbuka? Nahumu 1:5–8.**

---

"Mungu ni mvumilivu, hapendi mtu ye yote apotee; lakini ustahimilivu wake una mpaka, na ukipita mpaka, hakuna majaribio ya pili. Ghadhabu yake itatoka na ataangamiza bila dawa.

"Wakati wanadamu wakiwa madarakani, wanawadhulumu na kuwaharibu wanadamu wenzao, na hakuna mahakama ya kidunia inayoweza kupatikana kufanya haki, Mungu ataingilia kati kwa ajili ya wale ambao hawawezi kujitetea wenyewe. Ataadhibu kwa kila tendo la uonevu. Hakuna hekima ya kidunia inayoweza kuwalinda wakosaji dhidi ya hukumu za mbinguni.Na watu wanapoweka tumaini lao katika nguvu za kidunia badala ya Muumba wao, watakapokuwa na kiburi na kujiamini, Mungu kwa wakati Wake atawafanya wadharauliwe." — *The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 7, p. 946.

"Ulimwengu umekuwa na ujasiri katika uvunjaji wa sheria ya Mungu. Kwa sababu ya uvumilivu Wake wa muda mrefu, wanadamu wamekanyaga mamlaka Yake. Wametia nguvu wao kwa wao katika dhuluma na ukatili kwa urithi wake, wakisema, 'Mungu ajuaje? Yako maarifa kwake Aliye Juu?' Zaburi 73:11 . Lakini kuna mistari zaidi ambayo hawawezi kupita.Umekaribia wakati ambapo watakuwa wamefikia kikomo. Hata sasa wamekaribia kuvuka mipaka ya subira ya Mungu, mipaka ya neema yake, mipaka ya rehema zake. Bwana ataingilia kati ili kudhihirisha heshima yake mwenyewe, kuwakomboa watu wake, na kuzuia kuenea kwa uovu." — *Christ's Object Lessons*, pp.177,178.

**c. Tunajuaje kwamba dhambi haitatokea tena katika dunia mpya? Nahumu 1:9.**

---

## 4. TASWIRA LA KISASA

Jtan, Feb 25

**a. Ni tukio gani ambalo Nahumu anaonyesha likielekeza kwenye siku za mwisho kabla ya kurudi kwa Kristo—na jambo hilo linapaswa kutufanya tufikirie nini kuwa jambo la kwanza katika mazingira ya leo yenye mwendo wa kasi? Nahumu 2:3, 4; Yohana 9:4.**

---

---

"Piga kengele kupitia ardhi. Waambie watu ya kwamba siku ya Bwana i karibu, nayo inafanya haraka sana. Mtu yeyote asiachwe bila kuonywa. ....

"Hatuna muda wa kupoteza. Nguvu za giza zinafanya kazi kwa nguvu nyingi, na kwa kukanyaga kwa siri Shetani anasonga mbele kuwachukua wale ambao sasa wamelala, kama mbwa-mwitu anayekamata mawindo yake. Tuna maonyo sasa ambayo tunaweza kutoa, kazi ambayo tunaweza kuifanya sasa, lakini hivi karibuni itakuwa ngumu zaidi kuliko tunavyofikiria. . . .

"Kuja kwa Bwana kumekaribia kuliko tulipoanza kuamini. Pambano hilo kuu linakaribia mwisho wake. Kila ripoti ya maafa ya baharini au nchi kavu ni ushuhuda wa ukweli kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. Vita na uvumi wa vita vinatangaza. Je, kuna Mkristo ambaye mapigo yake ya moyo hayapigi kwa hatua ya haraka anapotarajia matukio makubwa yanayofunguliwa mbele yetu?

"Bwana anakuja. Tunasikia nyayo za Mungu anayekaribia, anapokuja kuiadhibu dunia kwa ajili ya uovu wake. Tunapaswa kumwandalia njia kwa kutenda sehemu yetu katika kuwatayarisha watu kwa ajili ya siku hiyo kuu." — *Evangelism,* pp.218, 219.

"Nguvu zote tulizopewa na Mungu, iwe ni ya mwili, akili, au kiroho, inapaswa kutumiwa kwa utakatifu kufanya kazi tuliyopewa kwa ajili ya wenzetu ambao wanaangamia katika ujinga wao." — *Testimonies for the Church,* vol.7,p.180.

"Kila mshiriki wa kanisa ambaye ana ujuzi wa Ukweli anatarajiwa kufanya kazi wakati kungali mchana; kwa maana usiku waja, asipoweza mtu kuifanya kazi." — *Ibid.*, vol. 9, p. 26.

**b. Eleza hatima ya wote wanaokataa rehema ya Mungu—kupokea ghadhabu Yake, kama inavyoonyeshwa kuelekea Ninawi katika Ashuru. Nahumu 2:8–11.**

---

"Kwa usahihi usio na kipimo Yule Asiye na kikomo bado anaweka hesabu na mataifa. Huku rehema yake inapotolewa, pamoja na miito ya toba, hesabu hii inabaki wazi; lakini takwimu zinapofikia kiwango fulani ambacho Mungu ameweka, huduma ya ghadhabu yake huanza. Hesabu imefungwa. Uvumilivu wa kimungu hukoma. Rehema haiwaombei tena." — *Prophets and Kings,* p. 364.

## 5. HISTORIA HUJIRUDIA — Alh, Feb 26

**a. Anguko la Ashuru linaonyeshwaje—na kwa nini jambo hili linafaa hasa sasa? Nahumu 3:7, 12, 13, 18, 19 .**

---

---

"Utukufu wa milki ya Ashuru ulikuwa mkuu; kubwa lilikuwa anguko lake." —*Prophets and Kings*, p. 365.

"Kiburi cha Ashuru na anguko lake vitatumika kama somo la kitu hadi mwisho wa nyakati. Katika mataifa ya dunia leo, ambao kwa kiburi na majivuno hujipanga kinyume chake, Mungu anauliza, 'Umefanana na nani hivi katika utukufu na ukuu kati ya miti ya Edeni? lakini utashushwa pamoja na miti ya Edeni hata pande za chini za nchi." — *Ibid.*,p.366.

**b. Tukio kama hilo litatokeaje hivi karibuni? Ufunuo 18:7–11, 15–18 .**

---

"[Ufunuo 18:11, 3, 15–17 imenukuliwa] Haya ndiyo maangamizi yanayomjia Babeli katika siku ya kujiliwa na ghadhabu ya mungu. Amejaza kipimo cha maovu yake; wakati wake umefika; ameiva kwa ajili ya kuangamizwa.

"Wakati sauti ya Mungu inapobadilisha wake wake walio mateka, kuna hali ya kutisha ya kuamsha wale waliopoteza kila kitu katika pambano kuu la maisha. Wakati muda wa rehema uliendelea kuwapo wao walipofushwa na madanganyo ya Shetani, na waliihalalisha njia yao ya dhambi. Matajiri walijivunia kuwa juu ya wale waliokuwa wamejaliwa kidogo; lakini walikuwa wamepata utajiri wao kwa kuivunja sheria ya Mungu. Walikuwa wamepuuza kuwalisha wenye njaa, kuwavika nguo walio uchi, kutenda kwa haki, na kupenda kuwa na huruma. Walikuwa wamejitahidi kujitukuza wenyewe na kutafuta kutukuzwa na viumbe wenzao. Sasa wameondoshewa vitu vyote vilivyowafanya wawe wakubwa na wameachwa wasio na kitu wala kinga. Wanatazama kwa hofu kuu kuangamizwa kwa sanamu ambazo walipenda zaidi kuliko Mwumbaji wao." — *The Great Controversy,* pp.653,654.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI — Ijum, Feb 27

1. Kulingana na Mika 6:8 , ni mambo gani matatu sahili tunayohitaji kufanya?
2. Kwa nini tu kuna tumaini hata kwa mwenye dhambi mbaya zaidi?
3. Kwa nini unyenyekevu ni sifa ya lazima ambayo Mungu anathamini, hasa leo?
4. Kwa kuwa wengi leo wamehukumiwa hatima ya Ninawi, tunapaswa kutanguliza nini?
5. Kuanguka kwa Babiloni kunahusianaje na kupuuzwa kwa Mika 6:8 ?

# Sadaka za Sabato ya Kwanza

Sabato, Marchi 7, 2026

**Field ya Maranhão Piauí (AMAPI)**

**Makao Makuu, Brazili**



Kaskazini-mashariki mwa Brazili, majimbo ya Maranhão na Piauí, kwa pamoja, yana wakaaji wapatao milioni 10.4, yaliyoenea katika eneo la takriban maili za mraba 224,282 (581,406 km2). Hali ya hewa hapa inaanzia ikweta hadi kitropiki hadi nusu kame, ikiwa na uoto wa asili wa mitende, mikoko, msitu wa Amazoni, cerrado na caatinga.

Kanisa la kwanza katika harakati ya matengenezo katika eneo hili lilianzishwa mwaka wa 1960, katika jiji la Bacabal, Maranhão. Pamoja na ukuaji wa idadi ya washiriki na kuanzishwa kwa makanisa mapya katika majimbo haya, Field ya Maranhão Piauí (AMAPI) ilipangwa mwaka wa 2016 ikiwa na washiriki wapatao 530.

Kama Field, tunahitaji kujenga ofisi za usimamizi, makao, na ukumbi. Ili kukamilika kwa makao makuu mapya, tunatumaini ukarimu na ukarimu wa ndugu na dada zetu wapendwa kutoka ulimwenguni pote.

“Mungu hategemei wanadamu kwa ajili ya kuendeleza kazi yake.

Angeweza kuwafanya malaika mabalozi wa ukweli wake. Angeweza kudhihirisha mapenzi yake, kama alivyoitangaza sheria kutoka Sinai kwa sauti yake mwenyewe. Lakini ili kusitawisha roho ya ukarimu ndani yetu, Amechagua kuwaajiri wanadamu kufanya kazi hii. Kila tendo la kujidhabihu kwa ajili ya manufaa ya wengine litaimarisha roho ya ufadhili katika moyo wa mtoaji, likimunganisha kwa ukaribu zaidi na Mkombozi wa ulimwengu, ambaye ‘alikuwa tajiri, lakini kwa ajili yetu akawa maskini, ili sisi kwa umaskini wake tuwe matajiri.’Na ni pale tu tunapotimiza kusudi la Mungu katika uumbaji wetu ndipo maisha yanaweza kuwa baraka kwetu. Zawadi zote njema za Mungu kwa mwanadamu zitathibitisha tu laana, isipokuwa atazitumia kuwabariki wanadamu wenzake, na kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Mungu duniani.” — *The Review and Herald*, December 7, 1886.

Ombi hili linapokufikia, tafadhali kumbuka baraka zinazoangukia msimamizi mwaminifu na ushirikiane nasi kwa fadhili katika jitihada hii—ambayo kwa neema ya Mungu itakuwa ya umuhimu mkubwa kwa ukuzi na kuendelea kwa kazi katika Nyanja hii. “Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu” (2 Wakorintho 9:7).

*Ndugu na dada zenu kutoka Field ya Maranhão Piauí*

SABATO, MARCHI 7, 2026

**Somo la 10**

# Heshima kwa Mwenye kujua yote

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Bwana yumo ndani ya hekalu lake takatifu, dunia yote na inyamaze kimya mbele zake" (Habakuki 2:20).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol.5, pp.491–500.

"Heshima ndani ya nyumba ya Bwana imekaribia kutoweka.... Tuna sababu nyingi za kuwa na bidii, na kujitoa wakfu kwelikweli katika ibada ya Mungu. Tunazo sababu nyingi za kufikiri na kuwa watu wenye heshima na kicho zaidi katika ibada zetu hata kuliko ilivyokuwa kwa Wayahudi." — *Testimonies for the Church*, vol.5, p.495.

## 1. SWALI KUBWA

**Jpil, Mar 1**

a. Nabii Habakuki alisema nini katika sala yake ya mwanzo kwa Mungu? Habakuki 1:1–4.

"Kwa maoni ya kibinadamu kusudi la kimungu kwa taifa lililochaguliwa lilionekana kuwa lisilowezekana kabisa kutimizwa. Ukengeufu wa karne za zamani ulikuwa umekusanya nguvu kwa miaka iliyopita; kumi ya makabila yalikuwa yametawanyika kati ya mataifa; ni makabila ya Yuda na Benjamini pekee yaliyosalia, na hata haya sasa yalionekana kwenye ukingo wa uharibifu wa kiadili na kitaifa.Manabii walikuwa wameanza kutabiri uharibifu kamili wa jiji lao zuri, mahali palipokuwa hekalu lililojengwa na Sulemani, na mahali ambapo matumaini yao yote ya kidunia ya ukuu wa taifa yalikuwa yamekazia. Je, inawezekana kwamba Mungu alikuwa karibu kugeuka kando kutoka kwa kusudi Lake lililo wazi la kuleta ukombozi kwa wale ambao walipaswa kuweka tumaini lao Kwake?Mbele ya manyanyaso ya muda mrefu ya wenye haki, na ufanisi yanaoonekana ya waovu, je, wale ambao walikuwa wamebaki waaminifu kwa Mungu wangeweza kutumainia siku bora zaidi? Maswali hayo yenye wasiwasi yalitolewa na nabii Habakuki." — *Prophets and Kings*, pp.384,385.

b. Bwana alijibu vipi? Habakuki 1:6–11.

## 2. UVUMILIVU KATIKA KUSUBIRI

Jtat, **Mar 2**

**a. Kwa nini Habakuki alikuwa tayari kukubali mpango wa Mungu? Habakuki 1:12, 13 .**

"Mungu alijibu kilio cha watoto wake waaminifu. Kupitia kinywa Chake alichochagua alifunua azimio Lake la kuleta adhabu juu ya taifa ambalo lilikuwa limemwacha na kutumikia miungu ya mataifa. Katika wakati wa maisha ya watu fulani ambao hata wakati huo walikuwa wakifanya uchunguzi kuhusu wakati ujao, Yeye angerekebisha kimuujiza mambo ya mataifa yanayotawala duniani na kuwaleta Wababeli katika ukuu. Wakaldayo hao, 'waliotisha na wa kuogofya,' wangeanguka ghafula juu ya nchi ya Yuda kama tauni iliyowekwa na kimungu." — *Prophets and Kings*, p.385.

**b. Ni somo gani lililotolewa kwa nabii lilitumika sana katika uzoefu wa waanzilishi wa awali wa Majilio? Habakuki 2:1–4.**

"Wakati ulipopita muda ambao Bwana alitazamiwa kuja, - katika majira ya kuchipua ya mwaka wa 1844, - wale waliokuwa wametazamia kwa imani kuja kwake waliingiwa na mashaka na wasiwasi kwa kipindi fulani. Wakati ulimwengu uliwaona kama watu waliokuwa wameshindwa vibaya na kuthibitika kuwa ni watu waliofuata udanganyifu, chanzo chao cha faraja bado kilikuwa ni neno la Mungu. Wengi waliendelea kuyachunguza Maandiko, wakiuchunguza upya ushahidi wa imani yao na kujifunza unabii kwa makini ili kupata nuru zaidi.. . . .

"katika unabii ambao walikuwa wameuchukulia kuhusiana na wakati wa marejeo, na walitiwa moyo kusubiri kwa uvumilivu katika imani kwamba kile kilichokuwa giza sasa katika ufahamu wao kingeweza kufanywa kuwa wazi kwa wakati wake. Miongoni mwa unabii huo ulikuwa ule wa Habakuki 2:1-4.....

"Mapema kadiri ya mwaka 1842 maagizo yaliyotolewa katika unabii huo ya "kuiandika njozi na kuifanya iwe wazi sana katika vibao, ili asomaye apate kuisoma kama maji," yalikuwa yamependekeza kwa Charles Fitch matayarisho ya mchoro wa chati ya unabii unaoelezea maono ya Danieli na Ufunuo. Kuchapishwa kwa mchoro ule kulichukuliwa kwamba ni kutimizwa kwa agizo la Habakuki. Hata hivyo, hakuna aliyeng'amua kwamba kuchelewa kule kwa dhahiri katika kutimizwa kwa njozi ile - kipindi cha kusubiri unabii huo huo." — *The Great Controversy*, pp.391,392.

a. Je, Habakuki 2:4 imewaimarishaje waumini katika kila kizazi? Warumi 1:16, 17 .

---

"Imani iliyomtia nguvu Habakuki na watakatifu na waadilifu wote katika siku hizo za majaribu makubwa ilikuwa imani ileile inayowategemeza watu wa Mungu leo. Katika saa zenye giza kuu, chini ya hali mbaya zaidi, muumini Mkristo anaweza kuiweka roho yake juu ya chanzo cha nuru na nguvu zote. Siku baada ya siku, kupitia imani katika Mungu, tumaini lake na ujasiri vinaweza kufanywa upya. 'Mwenye haki ataishi kwa imani yake.' Katika utumishi wa Mungu hapahitaji kuwa na hali ya kukata tamaa, wala kuyumbayumba, wala woga. . . .

"Lazima tuthamini na kusitawisha imani ambayo manabii na mitume wameshuhudia—imani ambayo inashikilia ahadi za Mungu na kungoja ukombozi katika wakati na njia Yake aliyoiweka." — *Prophets and Kings,* pp.386,387.

b. Tunapojaribiwa kutia shaka au kuangukia mawazo ya kujitumainisha kupitia kiasi, ni nini tunachopaswa kukikumbuka daima? Maombolezo 3:25, 26; Habakuki 2:20.

---

"Wakati wa kungoja unaweza kuonekana kuwa mrefu, roho inaweza kukandamizwa na hali za kukatisha tamaa, wengi ambao imani yao imewekwa wanaweza kuanguka njiani; lakini pamoja na nabii aliyejitahidi kuwatia moyo Yuda katika wakati wa uasi-imani usio na kifani, na tutangaze kwa uhakika, 'Bwana yu ndani ya hekalu lake takatifu; dunia yote na ikae kimya mbele zake." — *Ibid.*, pp.387,388.

"Heshima ya kweli kwa Mungu inaongozwa na hisia ya ukuu Wake usio na kikomo na utambuzi wa uwepo Wake." — *Education*, p.242.

"'Jina lake ni takatifu na la kustahiki.' Zaburi 111:9 , Malaika, wanenapo hilo, hufunika nyuso zao. Ni kwa heshima gani sisi, tulioanguka na wenye dhambi, tunapaswa kuichukua midomoni mwetu!

"Tunapaswa kuliheshimu Neno la Mungu. Kwa kiasi kilichochapishwa tunapaswa kuonyesha heshima, bila kukitumia kamwe kwa matumizi ya kawaida, au kukishughulikia kwa uzembe." — *Child Guidance*, p. 538.

"Wazazi, kuwa makini ni mfano gani na mawazo gani mnawapa watoto wenu. Akili zao ni za plastiki, na hisia zinafanywa kwa urahisi. Kuhusiana na huduma ya patakatifu, ikiwa mzungumzaji ana dosari, ogopa kutaja. Zungumza tu juu ya kazi nzuri anayofanya, juu ya mawazo mazuri aliyotoa, ambayo unapaswa kuzingatia kama yanakuja kupitia wakala wa Mungu.Inaweza kuonekana kwa urahisi ni kwa nini watoto wanavutiwa kidogo sana na huduma ya Neno na kwa nini wanakuwa na heshima ndogo sana kwa nyumba ya Mungu. Elimu yao imekuwa na kasoro katika suala hili." — *Ibid.,* p. 545.

## 4. KADIRI MAJARIBU YANAVYOZIDI.... Jtan, **Mar 4**

a. Je, ni sala gani ya bidii ya Habakuki tunayopaswa kurudia leo? Habakuki 3:2.

---

---

"Kuna uhitaji leo wa uamsho wa dini ya kweli ya moyo kama ule uliowahi kushuhudiwa na Israeli ya kale. Toba ni hatua ya kwanza ambayo lazima ichukuliwe na wote ambao wangemrudia Mungu.Hakuna mtu anayeweza kufanya kazi hii kwa mwingine. Ni lazima kila mmoja wetu anyenyekee nafsi zetu mbele za Mungu na kuiondoa miungu Tukiisha kufanya yote tuwezayo, Bwana atatudhihirishia wokovu wake." — *Patriarchs and Prophets*, p.590.

b. Hata tunapokabili matatizo makubwa na magumu , ni kitu gani kinachopaswa kuibainisha imani yetu kila wakati—na kwa nini? Habakuki 3:17–19; Wafilipi 2:14, 15 .

---

---

"Aliyeonewa sana, na aliyejaribiwa sana na aseme, 'Ingawa ataniua, nitamtumaini Yeye."—CounselstoParents,Teachers,andStudents,p.317.

"Damu ya Kristo inayosihi imemkinga mwenye dhambi asipate kipimo kamili cha hatia yake; lakini katika hukumu ya mwisho, ghadhabu inamiminwa pasipo kuchanganywa na rehema. . . .

"Watu wa Mungu hawatakuwa huru na maumivu; lakini wakiwa wanateswa na kupata dhiki, wakiwa wanastahimili umaskini na kuteseka kwa kukosa chakula, hawataachwa waangamie. Mungu yule aliyemtunza Eliya hatampita mmojawapo wa watoto wake aliyejitoa. Yeye azihesabuye hata nywele za kichwa chao atawatunza, na wakati wa njaa watashibishwa. Wakati waovu wanakufa kwa njaa na tauni, malaika watawalinda wenye haki na kuwapatia mahitaji yao." — *The Great Controversy*, p.629.

c. Ni nabii gani mwingine aliyeinuliwa katika kipindi hiki ili kuleta jumbe muhimu pia kwa wakati wetu? Sefania 1:1.

---

"Habakuki hakuwa peke yake ambaye kupitia kwake alipewa ujumbe wa tumaini angavu na la ushindi wa wakati ujao na vilevile wa hukumu ya wakati huu." Wakati wa utawala wa Yosia neno la Bwana lilimjia Sefania, likieleza waziwazi matokeo ya uasi-imani unaoendelea, na kuelekeza fikira za kanisa la kweli kwenye tazamio tukufu zaidi ya hapo. Unabii wake wa hukumu inayokuja juu ya Yuda unatumika kwa nguvu sawa na hukumu ambazo zitaangukia ulimwengu usio na toba wakati wa ujio wa pili wa Kristo." — *Prophets and Kings,* p.389.

## 5. MTEGO WA KUSIKITISHA NA ULIOFICHIKA — Alh, **Mar 5**

a. Ni ujumbe gani wenye uzito unaofunua ukweli wa hasira ya Mungu dhidi ya ibada ya uwongo na wale wanaoiendeleza? Sefania 1:2–6.

b. Ingawa mtu anaweza kudhania kuwa anamfuata Mungu, ni mitazamo gani inayofunua uasi mzito uliofichwa moyoni? Sefania 1:12, 13; Mathayo 24:48–51.

"Watu ambao Mungu amewakabidhi Ukweli mtakatifu, makini, unaojaribu kwa ajili ya wakati huu wamelala katika sehemu zao za kazi. Wanasema kwa matendo yao: Tunayo Kweli; sisi ni „matajiri, na tuna mali nyingi, na hatuhitaji chochote;" wakati Shahidi wa Kweli anatangaza: Nawe „hujui ya kuwa wewe ni mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.'

"Ni kwa uaminifu kiasi gani maneno haya yanaonesha hali ya sasa ya kanisa: „hujui ya kuwa wewe ni mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi." Ujumbe wa onyo, ulioamriwa na Roho Mtakatifu, unabebwa na watumishi wa Mungu, kasoro za tabia huwasilishwa mbele ya wakosaji; lakini wanasema: „Hilo haliwakilishi hali yangu. Sikubaliani na ujumbe mnaouleta. Ninafanya kadri niwezavyo. Ninaamini Ukweli.'

"Yule mtumwa mwovu aliyesema moyoni mwake, „Bwana wangu anakawia kuja, „alidai kumngojea Kristo. Alikuwa „mtumishi," kwa nje alijitolea kumtumikia Mungu wakati moyoni alikuwa amejisalimisha kwa shetani. Yeye haukani Ukweli waziwazi kama wale wa dhihaka, lakini maisha yake yanafunua hisia za moyo - kwamba kuja kwa Bwana kunacheleweshwa. Tabia ya kiburi inamfanya apuuzie masuala ya milele. Anazikubali kanuni za ulimwengu na kuambatana na desturi na mazoea yake. Ubinafsi, kiburi cha ulimwengu, na tamaa hutawala. Hali akiogopa kwamba ndugu zake wanaweza kuwa juu yake, anaanza kudharau juhudi zao na kuhoji makusudi yao. Kwa hiyo anawapiga watumishi/wajoli wenzake." — *Testimonies for the Church*, vol.5, pp.101,102.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI — Ijum, **Mar 6**

1. Ikiwa ninashangazwa na njia za Mungu, ni lazima nijifunze nini kutokana na sala za Habakuki?
2. Ni nani ninayejua ambaye angethamini chati ya matukio ya unabii?
3. Ni mambo gani ya mwenendo wangu katika nyumba ya Mungu yanapaswa kuboreshwa?
4. Kwa nini ni muhimu kwangu kupinga kishawishi cha kunung'unika na kulalamika?
5. Ninapokaripiwa, kwa nini ni muhimu kwangu kuwekeza katika uchunguzi wa kina wa moyo?

SABATO, MARCHI 14, 2026

Somo la 11

# Kukesha Kumtukuza Mungu

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Bwana wa majeshi asema hivi; Zitafakarini njia zenu" (Hagai 1:7).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol.9, pp.92–96.

"Usichelewe, lakini chunguza moyo wako kwa ukaribu na ufishe nafsi kila siku." — *Testimonies for the Churc*h, vol.3, p.336.

## 1. MAKUNDI MAWILI

Jpil, **Mar 8**

a.Eleza tukio tata litakalotokea hivi karibuni. Sefania 1:14–18.

"Wale wanaofanya kazi kwa hofu ya Mungu ili kuliondoa kanisa kwenye vizuizi na kurekebisha makosa mabaya, ili watu wa Mungu waone umuhimu wa kuchukia dhambi na kufaulu katika usafi, na ili jina la Mungu litukuzwe, watakutana daima na mivuto yenye kupinga kutoka kwa wale wasiojitakasa. Sefania anaielezea hali ya kweli ya watu wa daraja hili na hukumu za kutisha zitakazokuja juu yao:" — *Testimonies for the Church*, vol.3, pp.270, 271.

"[Zephaniah 1:2, 3, 8–18 imenukuliwa.]Kutakuwa na mfululizo wa matukio yanayodhihirisha kwamba Mungu Ndiye mtawala wa hali iliyopo. Ukweli utatangazwa kwa lugha iliyo wazi, isiyo na shaka. Kama watu lazima tuandae njia ya Bwana chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Injili inapaswa kutolewa katika usafi wake. Mto wa maji ya uzima unapaswa kuwa na kina na kupanuka katika mkondo wake. Katika mashamba yote, karibu na mbali, watu wataitwa kutoka kwenye ukulima na kutoka katika biashara za kawaida kabisa ambazo kwa kiasi kikubwa hutawala akili kwa kiasi kikubwa, na watafunzwa kwa kuunganishwa na watu wenye uzoefu. Kadri wanavyojifunza kufanya kazi kwa ufanisi watatangaza Kweli kwa nguvu. Kupitia kazi nyingi za ajabu za majaliwa ya Mungu, milima ya shida itaondolewa na kutupwa baharini. Ujumbe wenye maana sana kwa wakaaji wa duniani utasikiwa na kueleweka. Watu watajua Kweli ni nini. Mbele na mbele zaidi kazi itasonga mpaka dunia yote itakapoonywa, na ndipo ule mwisho utakapokuja." — *Ibid*., vol. 9, p. 96.

## 2. MATUNZO NA ULINZI

Jtat, **Mar 9**

a. **Ni nini ufunguo wa ulinzi wa Mungu katika shida inayokuja? Sefania 2:1–3, 15; 2 Wakorintho 7:1.**

---

---

---

"Mungu anawataka watu wake kujitakasa na uchafu wote wa mwili na roho, wakitimiza utakatifu katika kumcha Bwana. Wale wote ambao hawajali na wanajiondoa katika kazi hii, wakimngojea Bwana awafanyie yale ambayo Yeye anataka wayafanye wao wenyewe, wataonekana kupungua wakati yule mpole wa dunia, atakapokuwa amefanya hukumu zake zilizojificha ndani siku ya hasira ya Bwana." — *Testimonies for the Church,* vol.1,p.619.

"Katika siku ya Bwana, kabla tu ya kuja kwa Kristo, Mungu atatuma umeme kutoka Mbinguni katika ghadhabu yake, ambayo itaungana na moto duniani. Milima itawaka kama tanuru, na kumwaga vijito vya kutisha vya lava, kuharibu bustani na mashamba, vijiji na miji; na wanapomimina madini yao yaliyoyeyuka, miamba na matope ya moto kwenye mito, vitawafanya vichemke kama chungu, na kutuma mawe makubwa na kutawanya vipande vyao vilivyovunjika juu ya nchi kwa jeuri isiyoelezeka.Mito yote itakauka. Dunia itatikisika, na kutakuwa na milipuko ya kutisha na matetemeko ya ardhi kila mahali. Mungu atawapiga wakaaji waovu wa dunia mpaka waangamizwe kutoka humo. Watakatifu wamehifadhiwa duniani katikati ya machafuko haya ya kutisha, kama vile Nuhu alivyohifadhiwa ndani ya safina wakati wa gharika." — *Spiritual Gifts*, vol.3, pp.82,83.

b. **Tofauti na wale walio na taaluma duni, ni sifa gani waumini waaminifu wa Mungu? Sefania 3:1–4, 12, 13 .**

---

---

c. **Sefania anafunuaje tumaini kuu —na pia utume—kwa ajili ya watu waaminifu wa Mungu katika sehemu zote za ulimwengu? Sefania 3:14–16.**

---

---

"Mbingu zote hupendezwa, si tu katika nchi zilizo karibu na zinazohitaji msaada wetu, bali katika nchi zilizo mbali. Viumbe wa mbinguni wanatazama na kungoja mawakala wa kibinadamu waguswe sana na mahitaji ya wafanyikazi wenzao walio katika mashaka na majaribu, katika huzuni na dhiki." — *Testimonies for the Church*, vol.6, p.459.

## 3. FARAJA KWA WACHACHE WAAMINIFU — Jnne, **Mar 10**

**a. Ni maelezo gani yanayofichua kina cha upendo wa Mungu kwa watoto Wake—na jinsi tunavyopaswa kuuakisi? Sefania 3:17; 2 Wakorintho 1:3, 4 .**

---

---

"[Mungu] atakuleta katika nyumba yake ya karamu, na bendera yake juu yako ni mapenzi." ( Wimbo Ulio Bora 2:4 .'Ikiwa utatembea katika njia Zangu,' atangaza, 'nitakupa mahali pa kutembea kati ya hawa wanaosimama karibu'—hata kati ya malaika watakatifu wanaokizunguka kiti Chake cha enzi.... Na mbingu na nchi zitaungana katika wimbo wa Baba wa shangwe: 'Kwa maana huyu Mwanangu alikuwa amekufa, naye yu hai tena; alikuwa amepotea, naye amepatikana.'" — *Christ's Object Lessons*, pp.206,207.

"Malaika wa Mungu, maelfu kwa maelfu, na elfu kumi mara elfu kumi, wametumwa kuwahudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu. Wanatulinda dhidi ya uovu na kurudisha nyuma nguvu za giza ambazo zinatafuta uharibifu wetu. Je, hatuna sababu ya kuwa na shukrani kila wakati, wenye shukrani hata wakati kunapoonekana matatizo katika njia yetu?

"Bwana mwenyewe ndiye msaidizi wetu. „Imba, Ee binti Sayuni; piga kelele, Ee Israeli; furahi na kushangilia kwa moyo wote, Ee binti Yerusalemu." „Bwana, Mungu wako, Yu katikati yako shujaa, ataokoa, atakushangilia kwa furaha, atatulia katika upendo Wake, atakufurahia kwa kuimba." Sefania 3:14, 17Huu ndio shuhuda ambao Bwana anatamani sisi kuutoa kwa ulimwengu. Sifa Zake zinapaswa kuwa daima mioyoni mwetu na kwenye midomo yetu.

"Ushuhuda kama huo utakuwa na ushawishi kwa wengine. Tunapotafuta kuwageuza watu kutoka katika juhudi zao za kujitosheleza ili kupata furaha, lazima tuwaonyeshe kwamba tuna kitu bora kuliko kile wanachotafuta." — T*estimonies for the Church*, vol.6, pp.63,64.

**b. Elezea zaidi utunzaji wa upendo wa Mungu kwa watoto Wake wanaoteswa kwa kukataa kwao kukiuka sheria Yake ya uhuru. Sefania 3:18–20; Ezekieli 9:3, 4 .**

---

---

"Chunga jambo hili kwa uangalifu: Wale wanaopokea alama safi ya Ukweli, iliyotengenezwa ndani yao kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, iliyowakilishwa na alama ya mtu aliyevaa bafta, ni wale „wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yote yanayotendekakiasi kwamba wanawakilishwa kama wenye uchungu, na walio katika hali ya kuugua na kulia." — *Testimonies for the Church*, vol.3, p.267.

## 4. KUTATHIMINI NJIA ZETU

Jtan, **Mar 11**

a. **Hagai alipoitwa kuwa nabii, ni nini kilikuwa kikiendelea—na tunapaswa kujifunza nini kutokana na hali hiyo? Hagai 1:1–4 .**

---

"Usemi, 'Watu hawa wanasema,' ni wa maana. Katika saa ya nafasi yao, Waisraeli hawakuwa wamejionyesha kuwa tayari. Utiifu wa haraka unatarajiwa kwa wale ambao Bwana anawachagua na kuwaongoza. Maombi ya kucheleweshwa ni aibu kwa Mungu. Na bado wale wanaochagua kufuata njia zao wenyewe, mara nyingi huweka visingizio vya busara katika kujihesabia haki. Hivyo Waisraeli walitangaza kwamba walikuwa wameanza kujenga upya, lakini kwamba walikuwa wamevunjwa katika kazi yao kwa sababu ya vizuizi vilivyopangwa na adui zao. Vizuizi hivyo, walifikiri, vilikuwa dalili kwamba haukuwa wakati ufaao wa kujenga upya.Walitangaza kwamba Bwana ali- kuwa ameingilia matatizo ili kukemea haraka yao isiyo na busara. Hii ndiyo sababu, katika mawasiliano kupitia nabii Wake, Yeye aliwataja si 'watu wan- gu,' bali 'watu hawa.'

"Waisraeli hawakuwa na kisingizio cha kweli cha kuacha kazi yao katika hekalu. Wakati ambapo pingamizi kubwa zaidi lilitolewa, ulikuwa wakati wa wao kudumu katika kujenga. Lakini walichochewa na kutopenda ubinafsi kukutana na hatari kwa kuamsha upinzani wa adui zao.Hawakuwa na imani ambayo ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyoonekana. Walisita kusonga mbele kwa imani katika majaliwa ya Mungu ya ufunguzi, kwa sababu hawakuweza kuona mwisho tangu mwanzo.Matatizo yalipotokea, walikengeushwa kwa urahisi kutoka kwenye kazi hiyo." — *The SDA Bible Commentary [E.G.White Comments],* vol.4, p.1175.

b. **Ni wito gani unaotolewa kwa wale wanaokengeushwa na mambo ya kilimwengu? Hagai 1:5–10.**

---

"Kielelezo chenye kutokeza cha matokeo ya kunyima kwa ubinafsi hata matoleo ya hiari kutoka kwa kazi ya Mungu ilitolewa katika siku za nabii Hagai. .. .Wayahudi walichukua hatua ya kulijenga upya hekalu la Bwana; lakini walipokutana na upinzani mkali kutoka kwa adui zao, walikomesha kazi hiyo." — *Patriarchs and Prophets,* p. 527.

c. **Je, mabaki walipataje ushindi wa moyo na matendo? Hagai 1:12, 13 .**

---

"[Mabaki] hawakuthubutu kupuuza onyo la kurudiwa-rudiwa kwamba ufanisi wao na baraka za Mungu zilitegemea utii wao wote kwa maagizo waliyopewa.Mara tu walipoamua kwamba wangefanya maneno ya Bwana, jumbe Zake za karipio zilibadilika na kuwa maneno ya kutia moyo. Ee Mungu wetu ni mwingi wa rehema!" — *SDA Bible Commentary [E.G.White Comments],* vol.4, p.1176.

## 5. UTUKUFU KATIKA NJIA TOFAUTI — Alh, **Mar 12**

a. Eleza mpango wa Mungu kwa hekalu la pili ambalo lingejengwa. Hagai 2:6–9.

---

---

"Baada ya hekalu kuharibiwa na Nebukadnezar lilijengwa tena karibu miaka 500 kabla ya Kristo kuzaliwa. Lilijengwa na watu ambao walikuwa wamekaa utumwani kwa muda mrefu wa maisha yao na walikuwa wamerejea katika nchi iliyoharibiwa na kuachwa ukiwa. Walikuwemo miongoni mwao wazee ambao waliona utukufu wa hekalu la Sulemani, ambao walilia panapo msingi wa jengo hili jipya la hekalu, kwamba huenda hili likawa hafifu kuliko lile la awali. Hisia iliyokuwepo inaelezwa hapa na nabii: „Nani amesalia miongoni mwenu aliyeona nyumba hii katika utukufu wake wa kwanza? Na je mnaionaje sasa? Je machoni mwenu si mnaiona kama si kitu?" Hagai 2:3; Ezra 3:12. Hatimaye, ilitolewa ahadi kwamba utukufu wa nyumba hii ungekuwa mkubwa kuliko ule wa ile ya kwanza.

"Lakini hekalu la pili halikuwa na uzuri kama ule wa lile la kwanza; wala halikudhihirishwa na mwonekano wa kuwepo kwa Mungu kama ilivyokuwa katika hekalu la kwanza. Hakukuwa na udhihirisho wa nguvu na uweza ulioashiria kuwekwa wakfu kwake. Hakukuwa na wingu la utukufu lililojaza patakatifu. Hakuna moto ulioshuka madhabahuni kutoka mbinguni ili kuteketeza dhabihu. Hakukuwa na Shekina katikati ya makerubi katika patakatifu pa patakatifu; sanduku, kiti cha rehema, na meza za ushuhuda zisingeonekana mle ndani. Hakuna sauti iliyotoka mbinguni kuwajulisha makuhani mapenzi ya Yehova.

"Kwa karne nyingi Wayahudi walikuwa wametafuta pasipo mafanikio kuonyesha ikiwa ahadi ya Mungu aliyotoa kupitia Hagai ilikuwa imetimia; lakini kiburi na kutokuamini vilipofusha mawazo yao wasielewe maana halisi ya maneno ya nabii. Hekalu la pili halikujazwa na utukufu wa Yehova, isipokuwa kwa uwepo wake yeye aliye na ujazo wote wa Uungu – aliyekuwa Mungu mwenyewe akijidhihirisha katika mwili. Yeye aliye "Tumaini la mataifa yote" alikuwa amekuja katika hekalu lake wakati Mnazareti alipofundisha na kuponya. Katika uwepo wa Kristo, na katika huu tu, ndipo hekalu la pili lilipolizidi la kwanza kwa utukufu." — *The Great Controversy*, pp.23,24.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI — Alh, **Mar 13**

1. Katika hali ngumu inayokuja hivi karibuni, ninawezaje kuwa nguvu ya wema mikononi mwa Mungu?
2. Kwa nini upole ni sifa muhimu ya kutafuta katika siku hizi za mwisho?
3. Wote wanaofichwa katika siku ya hasira ya Bwana ni nini?
4. Ni nini huelekea kunifanya nipoteze kipaumbele cha kwanza maishani?
5. Kwa nini hekalu lililo sahili zaidi na duni lililojengwa katika siku za Hagai lilikuwa tukufu sana?

SABATO, MARCHI 21, 2026

Somo la 12

# Matukio ya Wakati wa Mwisho

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Mwombeni Bwanamvua wakatiwa masika; naam, Bwana afanyaye umeme, naye atawapa manyunyu ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni" (Zekaria 10:1).

**Inapendekezwa kusoma:** *Prophets and Kings*, pp.580–592; *Testimonies to Ministers*, pp.506–512; *The Acts of the Apostles*, pp.47–56.

"Tunapomtafuta Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu, itafanya kazi ndani yetu upole, unyenyekevu wa akili, kumtegemea Mungu kwa uangalifu kwa ajili ya mvua ya masika inayokamilisha. Tukiomba baraka kwa imani, tutaipokea kama Mungu alivyoahidi."—*TestimoniestoMinisters*,p.509.

## 1. MBONI YA JICHO LAKE

Jpil, **Mar 15**

a. Zekaria aliunga vipi ujumbe wa Hagai? Zekaria 1:1–4, 15, 16 .

"Maombi ya dhati na kutia moyo yaliyotolewa kupitia Hagai yalisisitizwa na kuongezewa na Zekaria, ambaye Mungu alimwinua kusimama upande wake katika kuwahimiza Israeli kutekeleza amri ya kusimama na kujenga. Ujumbe wa kwanza wa Zekaria ulikuwa uhakikisho kwamba neno la Mungu halishindwi kamwe na ahadi ya baraka kwa wale ambao wangesikiliza neno la hakika la unabii."—Prophets and Kings, p. 576.

b. Ni nini kinachofunua jinsi Mungu anavyowalea kwa makini watu Wake? Zekaria 2:1–5, 8 .

"Mungu alikuwa ameamuru kwamba Yerusalemu ijengwe upya;maono ya kupimwa kwa mji huo yalikuwa hakikisho kwamba angewapa faraja na nguvu watu wake walioteswa, na kuwatimizia ahadi za agano lake la milele.Utunzaji wake wa ulinzi, alitangaza, ungekuwa kama 'ukuta wa moto kuzunguka pande zote;' na kupitia kwao utukufu Wake ungefunuliwa kwa wana wote wa wanadamu. Alichokifanya kwa ajili ya watu wake kilipaswa kujulikana duniani kote." — *Ibid.*,p. 581.

## 2. UHITAJI WETU WA KRISTO

Jtat, **Mar 16**

**a. Tukiwa na kasoro, ni nini kinachoonyesha tumaini letu pekee? Zekaria 3:1–4.**

"Katika mfano wa unabii wa Zekaria, Shetani anaonekana akisimama mkono wa kuume wa Malaika wa Bwana, akimshtaki Yoshua, kuhani mkuu, aliyevaa mavazi machafu, naye Shetani anaipinga kazi ambayo Malaika wa Mungu anataka kumfanyia Yoshua. Hii huonesha nia aliyo nayo Shetani dhidi ya kila mtu ambaye Kristo ataka kumvuta kwake. " — *Thoughts From the Mount of Blessing*, pp.116, 117.

"[Shetani]kutuongoza ili tufikiri kwamba makosa yetu na dhambi zetu zimekuwa nzito sana hata Bwana hawezi kuzijali sala zetu, tena hawezi kutubariki na kutuokoa. Ndani yetu wenyewe hatuwezi kuona cho chote ila udhaifu tu, hakuna kitu cha kutupatia sifa kwa Mungu, na Shetani anatuambia kwamba hatuna matumaini tena; hatuwezi kufanya lo lote kurekebisha mapungufu ya tabia zetu. Tunapojaribu kumwendea Mungu, adui ananong'ona na kutuambia, "Ni kazi bure kwako kuomba; je, hivi hukufanya jambo lile baya? Je, hujatenda dhambi dhidi ya Mungu, na kuihalifu dhamiri yako?" Lakini, twaweza kumwambia yule adui ya kuwa "damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi zote." 1 Yohana 1:7. Tunapoona kwamba tumefanya dhambi, na hatuwezi kuomba, huo ndio wakati hasa wa kusali." — *Ibid*., p. 115.

**b. Ni kanuni gani ya kiungu inayofichua chanzo cha kweli cha nguvu za kushinda dhambi na kutimiza mwito wa Mungu? Zekaria 4:6; Yohana 15:5.**

"Kama watu wateule wa Mungu hatuwezi kuiga mazoea, malengo, au mitindo ya ulimwengu. Hatujaachwa gizani katika kuiga mifano ya kidunia na kutegemea muonekano wa nje kwa ajili ya mafanikio. Bwana ametuambia zinakotoka nguvu zetu[Zechariah4:6imenukuliwa.]" — *Testimonies for the Church*, vol.7, p.90.

"Bila Roho wa Mungu ujuzi wa neno lake haufai kitu. Nadharia ya ukweli, bila kuandamana na Roho Mtakatifu, haiwezi kuhuisha nafsi au kutakasa moyo. Mtu anaweza kuwa anafahamu amri na ahadi za Biblia; lakini Roho wa Mungu asipoiweka kweli nyumbani, tabia haitabadilishwa.Bila kuangaziwa na Roho, wanadamu hawataweza kutofautisha ukweli na uwongo, na wataanguka chini ya majaribu makuu ya Shetani." — *Christ's Object Lessons*, pp.410,411.

"Katika karama kuu na isiyo na kipimo ya Roho Mtakatifu zimo rasilimali zote za mbinguni…. Kama wote wangekuwa tayari kupokea, wote wangejazwa na Roho wake." — *Ibid.,*p.419.

## 3. AINA TOFAUTI YA HEKALU

**Jnne, Mar 17**

a. **Taja hekalu muhimu zaidi ambalo lingejengwa—na nani. Zekaria 6:12, 13, 15; Waefeso 2:19–22.**

---

"Juu ya msingi ambao Kristo mwenyewe alikuwa ameuweka, mitume walijenga kanisa la Mungu. Katika Maandiko kielelezo cha kusimamishwa kwa hekalu kinatumika mara kwa mara kuelezea ujenzi wa kanisa. Zekaria anamrejelea Kristo kama Tawi linalopaswa kujenga hekalu la Bwana.Asema juu ya Wasio Wayahudi wanaosaidia katika kazi: 'Nao walio mbali watakuja na kujenga katika hekalu la Bwana;' na Isaya atangaza, 'Na wageni watajenga kuta zako.' Zekaria 6:12, 15; Isaya 60:10.

"Akiandika juu ya ujenzi wa hekalu hili, Petro asema, 'Yeye akija kwake, kana kwamba kwa jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima; ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.' ( 1 Petro 2:4, 5 ).

"Katika machimbo ya ulimwengu wa Wayahudi na Wamataifa mitume walifanya kazi kwa bidii, wakitoa mawe ya kuwekwa juu ya msingi." —*The Acts of the Apostles,* pp.595,596.

b. **Licha ya maonyo ya Mungu, watu walikuwa wamefanya nini kabla ya utekwa wao? Zekaria 7:8–14.**

---

c. **Je, Mungu alionyeshaje hata hivyo kumiminiwa kwa rehema ya ustahimilivu katika kutoa fursa baada ya fursa? Zekaria 8:7, 8, 13–17 .**

---

"Lilikuwa bado kusudi la Bwana, kama lilivyokuwa tangu mwanzo, kwamba watu wake wawe sifa duniani, kwa utukufu wa jina lake. Wakati wa miaka mingi ya uhamisho wao alikuwa amewapa fursa nyingi za kurudi kwenye utii wao Kwake.Wengine walikuwa wamechagua kusikiliza na kujifunza; wengine walikuwa wamepata wokovu katikati ya dhiki. Wengi wa hawa walipaswa kuhesabiwa miongoni mwa mabaki ambao wangerudi." — *Prophets and Kings*, p. 599.

"[Zekaria 8:3, 7, 8 iliyonukuliwa.] Ahadi hizo zilitegemea utii." Dhambi ambazo Waisraeli walikuwa nazo kabla ya utekwa hazikupaswa kurudiwa tena." — *Ibid*, p. 704.

## 4. HITAJI LA KUBURUDISHA

Jtan, **Mar 18**

**a. Sasa katika wakati huu katika historia, ni nini kinapaswa kuwa lengo letu, na kwa nini hii ni muhimu sana? Zekaria 10:1, 2 .**

---

"Washiriki wa kanisa la Mungu leo wawe na muunganisho hai na Chanzo cha ukuaji wote wa kiroho, hawatakuwa tayari kwa wakati wa kuvuna." — *The Acts of the Apostles*, p. 55.

"'Ombeni mvua kwa Bwana wakati wa mvua ya masika.' Usipumzike kuridhika kwamba katika mwendo wa kawaida wa majira, mvua itanyesha. Uliza. Ukuaji na ukamilifu wa mbegu hautegemei mkulima. Mungu pekee ndiye anayeweza kuivisha mavuno. Lakini ushirikiano wa mwanadamu unahitajika. Kazi ya Mungu kwa ajili yetu inadai utendaji wa akili zetu, matumizi ya imani yetu.Ni lazima tutafute neema zake kwa moyo wote ikiwa manyunyu ya neema yatakuja kwetu.Tunapaswa kuboresha kila fursa ya kujiweka katika njia ya baraka. Kristo amesema, 'Walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.' Mikusanyiko ya kanisa, kama vile katika mikutano ya kambi, mikusanyiko ya kanisa la nyumbani, na nyakati zote ambapo kuna kazi ya kibinafsi kwa ajili ya nafsi, ni fursa zilizowekwa na Mungu za kutoa mvua ya kwanza na ya masika.

"Lakini mtu yeyote asifikirie kwamba katika kuhudhuria mikusanyiko hii, wajibu wao umekamilika. Kuhudhuria tu mikutano yote inayofanywa peke yake hakuwezi kuleta baraka kwa nafsi. Sio sheria isiyobadilika kwamba wote wanaohudhuria mikusanyiko mikuu au mikutano ya mtaa watapata mahitaji makubwa kutoka mbinguni.Hali inaweza kuonekana kuwa nzuri kwa kumiminiwa kwa wingi kwa manyunyu ya neema. Lakini Mungu mwenyewe lazima aamuru mvua inyeshe. Kwa hiyo tusiwe wazembe katika kuomba." — *Testimonies to Ministers*, pp.508,509.

**b. Eleza tukio la kushangaza kutokea chini ya mamlaka hii. Zekaria 12:8.**

---

"Wakati miti isiyo na matunda inapokatwa kwamba inaitaabisha lishe ya ardhi bure, wakati idadi kubwa ya ndugu wa uongo inapotofautishwa na ile ya Kweli, basi wale waliofichwa watafunuliwa kutazamwa, na kusanyiko la waimba hosana chini ya bendera ya Kristo. Wale ambao wamekuwa waoga na wasiojiamini watajitangaza waziwazi kwa ajili ya Kristo na Ukweli Wake. Wanyonge zaidi na wanaosita kanisani watakuwa kama Daudi - aliye tayari kufanya na kuthubutu. Kadiri usiku unavyokuwa mwingi kwa watu wa Mungu, ndivyo nyota zinavyong'aa zaidi. Shetani atawatesa sana waaminifu; lakini, kwa Jina la Yesu, watatoka wakiwa zaidi ya washindi"— *Testimonies for the Church*, vol.5, p.81.

## 5. KRISTO KATIKA UZIMA WA MILELE — Alh, **Mar 19**

a. **Eleza moja ya mazungumzo mazuri yajayo milele. Zekaria 13:6.**

---

"Yesu ataonyesha mikono yake yenye alama ya kusuliuniwa kwake. Alama hizi za ukatili daima atakuwa nazo. Kila alama ya msumari itaeleza historia ya ukombozi wa ajabu wa mwanadamu na gharama ya thamani iliyoununua." — *Early Writings*, p. 179.

b. **Kristo atarudi lini na jinsi gani kwenye Mlima wa Mizeituni, na ni matukio gani makubwa sana yatakayotokea? Zekaria 14:4,5; Ufunuo 20:7, 12; 21:2, 10 .**

---

"[Malaika alieleza:]"Watakatifu watastarehe katika mji mtakatifu na kuumiliki kama wafalme na makuhani kwa muda wa miaka elfu moja, Kisha Yesu atashuka pamoja na watakatifu juu yam lima wa mizeituni, na mlima huo utapasuka Mara mbili na kuwa tambarare kubwa kwa ajili ya Paradiso ya Mungu kukaa. " — *Ibid*., pp.51,52.

"Mwishoni mwa miaka elfu moja, Yesu, Mfalme wa Utukufu, anashuka kutoka kwenye Jiji Takatifu, akiwa amevikwa mwangaza kama umeme, juu ya Mlima wa Mizeituni—mlima uleule alikopanda baada ya kufufuka Kwake.Miguu Yake inapougusa mlima, unagawanyika, na kuwa tambarare kubwa sana, na unatayarishwa kwa ajili ya kuupokea Mji Mtakatifu ambao ndani yake kuna paradiso ya Mungu, bustani ya Edeni, ambayo ilichukuliwa baada ya kosa la mwanadamu. Sasa inashuka na mji, mzuri zaidi, na kupambwa kwa utukufu kuliko wakati kuondolewa kutoka duniani.Mji wa Mungu unashuka na kukaa juu ya bonde kuu lililoandaliwa kwa ajili yake. Kisha Yesu anauacha mji ukiwa umezungukwa na jeshi lililokombolewa, na anasindikizwa katika njia Yake na umati wa malaika. Kwa ukuu wa kutisha huwaita wafu waovu. Wanaamshwa kutoka katika usingizi wao mrefu. Uamsho wa kutisha kama nini!" — *Spiritual Gifts*, vol. 3, p. 83.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI — Ijum, **Mar 20**

1. Kuonyesha "ukuta wa moto" ambao Mungu anaahidi, ni wakati gani nimehisi ulinzi Wake?
2. Kwa nini ninaweza kutupilia mbali mashambulizi ya Shetani ambayo yanaonyesha dhambi zangu mbele yangu?
3. Ni nini kilicho muhimu zaidi kuliko hekalu halisi la kuweka uwepo wa Mungu?
4. Taja baadhi ya mahitaji muhimu ili kupokea Mvua za Masika.
5. Miguu ya Yesu itasimama lini tena kwenye Mlima wa Mizeituni?

SABATO, MARCHI 28, 2026

Somo la 13

# Ombi la Mwisho la Malaki

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa; naye atawatakasa wana wa Lawi, na atawasafisha kama dhahabu na fedha, nao watamtolea Bwana dhabihu katika haki" (Malaki 3:3).

**Inapendekezwa kusoma**: *Prophets and Kings*, pp.702–721;
*Testimonies for the Church*, vol.7, pp.45–50.

"Watenda maovu wa kusikitisha walionywa juu ya siku ya hukumu inayokuja na juu ya kusudi la Yehova la kuwafikia maangamizi ya haraka kila mvunjaji wa sheria. Walakini hakuna aliyeachwa bila tumaini; Unabii wa Malaki wa hukumu uliandamana na mialiko kwa wasiotubu wafanye amani yao pamoja na Mungu." — *Prophets and Kings*, p. 706.

## 1.MAKOSA YANAYOPUUZWA MARA NYINGI

Jpil, **Mar 22**

a. Ni mwenendo upi wa tama binafsi ambao tunaweza kuwa na hatia yake? Malaki 1:8.

---

---

"Wengi wamejiingiza kwenye gharama isiyo ya lazima, ili tu kuridhisha hisia, tamaa, na macho, wakati kazi ilihitaji mali hizo hizo zilizotumika katika mambo hayo, na wakati baadhi ya watumishi wa Mungu wakiwa wamevaa vibaya na wakiwa vilema katika utumishi wao kwa kukosa mali. Malaika alisema: "Wakati wao wa kufanya hivi upo karibu kwisha. Kazi zao zinaonesha kuwa ubinafsi ni sanamu yao, na wanatoa kafara kwao." Ubinafsi ni lazima kwanza uridhishwe; hisia zao ni: "Je! mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" Wengi wamepokea onyo baada ya onyo, lakini hawakutii. Ubinafsi ndiyo lengo kuu, na kila kitu lazima likubali hilo" — *Testimonies for the Church*, vol. 1, p. 115.

b. Tofauti kabisa na desturi za jamii ya leo, Mungu huonaje ahadi muhimu na takatifu ya ndoa? Malaki 2:12–16; Waebrania 13:4; Mathayo 19:4–6.

---

"Jifunzeni ili kuendeleza furaha ya kila mmoja. Wacha kuwe na upendo wa pande zote, uvumilivu wa pande zote. Kisha ndoa, badala ya kuwa mwisho wa upendo, itakuwa kama ilivyokuwa mwanzo wa upendo." — *The Ministry of Healing*, p.360.

## 2. MCHAKATO WA KUSAFISHWA

Jtat, **Mar 23**

### a. Eleza utimizo wa kinabii wa Malaki 3:1–3; Yohana 2:13–16.

---

"Katika kule kutakasa hekalu, Yesu alikuwa anatangaza kazi yake kama Masihi, na alikuwa akiingia katika kazi yake....Mahakama za hekalu la Yerusalemu, vilivyojawa na fujo za biashara isiyo takatifu, viliwakilisha kwa usahihi kabisa hekalu la moyo, ambalo limechafuliwa na uwepo wa hisia za tamaa na mawazo yasiyo na utakatifu. Katika kule kusafisha hekalu kutokana na wauzaji na wanunuzi wa kiulimwengu, Yesu alitangaza kazi yake ya kusafisha moyo kwa kuondoa uchafu wa dhambi, - kutokana na tamaa ya mambo ya kidunia, ubinafsi, tabia za uovu, ambazo zinaharibu roho." — *The Desire of Ages,* p. 161.

"Mungu angependa watumishi Wake wafahamu mitambo ya maadili ya mioyo yao. Ili kuleta jambo hili, Yeye mara nyingi huruhusu moto wa taabu kuwashambulia ili wapate kutakaswa....."

"Utakaso wa watu wa Mungu hauwezi kutimizwa bila mateso yao. Mungu anaruhusu moto wa mateso kuteketeza taka, kutenganisha visivyo na thamani na vya thamani, ili chuma safi kiangaze. Hutupitisha kutoka kwa moto mmoja hadi mwingine, akijaribu thamani yetu ya kweli. Ikiwa hatuwezi kuvumilia majaribu haya, tutafanya nini wakati wa taabu? Ustawi au shida zikigundua uwongo, kiburi, au ubinafsi ndani ya mioyo yetu, tutafanya nini wakati Mungu akapojaribu kazi ya kila mtu kama kwa moto, na kufunua siri za mioyo yote?" — *Testimonies for the Church,* vol.4, p.85.

### b. Taja baadhi ya njia ambazo watu wa Mungu wanakemewa kwa kumsahau, na kumwibia Mungu kunahusisha nini kwa kweli? Malaki 3:5–8; Yakobo 1:27; Luka 12:15; Mithali 3:9,10.

---

"Lazima tuamue kwa makusudi kwamba tutamheshimu Mungu kwa mali zetu; halafu hatupaswi kuruhusu chochote kitushawishi kumnyang'anya Zaka na matoleo ambayo ni haki Yake. Lazima tuwe na akili, utaratibu, mkakati na kuendelea katika matendo yetu ya hisani kwa watu na mawazo yetu ya kumshukuru Mungu kwa neema Zake kwetu. Hili ni jukumu takatifu sana ambalo halipaswi kuachwa kwa bahati mbaya au kudhibitiwa na msukumo au hisia. Tunapaswa kuweka akiba ya kitu mara kwa mara kwa sababu ya Mungu, ili asiibiwe sehemu ambayo anadai. Tunapomwibia Mungu tunajiibia  wenyewe pia. Tunakosa hazina ya mbinguni kwa sababu ya kutafuta mambo ya dunia hii zaidi. Hii ni hasara ambayo hatuwezi kumudu kuendelea nayo. Ikiwa tunaishi ili tuweze kupata baraka za Mungu, basi mkono Wake unaofanikisha utakuwa pamoja nasi katika mambo yetu ya kidunia, lakini ikiwa mkono Wake uko kinyume chetu anaweza kuangusha mipango yetu yote na kuitawanyika haraka zaidi kuliko tunavyoweza kukusanya." — *Ibid,* vol.5, pp.271, 272.

## 3. KUMBUKUMBU ZA KINA

Jnne, **Mar 24**

**a. Taja baadhi ya baraka zinazotokana na kurudi kwa zaka ya uaminifu na matoleo ya ukarimu—na ueleze hitaji letu la kuepuka kuchelewa katika hili. Malaki 3:10–12 .**

---

"Lakini upendo na ukarimu huu wa kitanda cha mauti siyo ambao Kristo anauhitaji kwa wafuasi Wake; hauwezi kuwa udhuru wa ubinafsi wa walio hai. Wale ambao wanashikilia mali zao hadi wakati wa mwisho, wanazisalimisha kwa ajili ya kifo siyo kwa ajili ya kazi. Hasara zinatokea kila wakati. Mabenki yanapata hasara, na mali zinatumika kwa njia nyingi sana. Wengi wanakusidia kufanya kitu fulani, lakini wanachelewa, na Shetani anafanya kazi kuzuia mali isiingie kwenye hazina kabisa. Inapotea kabla haijarudishwa kwa Mungu, na shetani anafurahi kuwa hivyo.

"Endapo mtafanya mema kwa mali zenu, fanyeni mara moja shetani asije akazichukua mikononi mwake na hivyo kuizuia kazi ya Mungu. Mara nyingi, Bwana alipofungua njia kwa ajili ya ndugu zetu ili kuzitumia mali zao katika kuiendeleza kazi Yake, mawakala wa shetani wamewasilisha biashara ambayo walikuwa na uhakika kwamba ndugu hawa wangeweza kuongeza mali zao. Wanachukua chambo; pesa zao zinawekezwa, kisha kazi, na mara nyingi pamoja na wao wenyewe, hawapati hata shilingi moja." — *Testimonies for the Church*, vol.5,p.154.

**b. Ni kumbukumbu gani iliyo sahihi kwa uchungu tunapaswa kuazimia kuona ikifutiliwa mbali? Mhubiri 12:14; Isaya 65:6, 7 .**

---

---

**c. Zaidi ya kuwa na majina yao katika kitabu cha uzima, ni nini kinachofunua matendo katika kumbukumbu ya Mungu ya watoto Wake waaminifu? Malaki 3:16; Zaburi 56:8.**

---

"Kitabu cha Ukumbusho" kimeandikwa mbele za Mungu, ambamo ndani yake yameandikwa matendo mema ya "hao waliomcha BWANA, na kulitafakari jina lake." Malaki 3:16. Maneno yao ya imani, matendo yao ya upendo, yameandikwa mbinguni. Nehemia anarejea katika habari hiyo anaposema: "Unikumbukie hayo, Ee Mungu wangu,, . . .wala usifute fadhili zangu nilizozitenda kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu." Nehemia13:14. Katika kitabu cha Mungu cha ukumbusho kila tendo la haki lililofanywa linadumishwa. Kila jaribu lililopingwa, kila ovu lililolishindwa, kila neno la huruma lililonenwa, limeandikwa mle kwa uaminifu. Na kila tendo la kujitoa kafara, kila taabu na huzuni iliyostahimiliwa kwa ajili ya Kristo, yameandikwa mle" — *The Great Controversy*, p.481.

a. **Je, ni shangwe gani ambayo Mungu huonyesha kwa watu Wake waaminifu, na tunawezaje kuonyesha shangwe hiyo katika tabia na matendo yetu? Malaki 3:17; Mathayo 25:34–40.**

---

---

“Wakati unapohurumia mioyo iliyolemewa na kukatishwa tamaa kwa huzuni, wakati mkono unanyooshwa kwa wahitaji, wakati walio uchi wanavikwa, mgeni anakaribishwa kwenye kiti sebuleni kwako na anapewa nafasi moyoni mwako, malaika wanasogea karibu zaidi, na kila ombi lililoelekezwa mbinguni hujibiwa. Kila tendo la haki, huruma, na ukarimu huleta nyimbo mbinguni..”—Testimonies for the Church, vol. 2, p. 25.

b. **Tunajuaje kwamba tofauti kati ya waovu na waadilifu itadhihirika wazi hivi karibuni? Malaki 3:18; Ufunuo 22:11, 12 .**

---

“Na mbingu zitatangaza haki yake, kwa maana Mungu ndiye aliye hakimu.” Zaburi 50:6. Sheria ile takatifu, haki ya Mungu, ile iliyotangazwa katikati ya ngurumo na moto kutokea Sinai kama mwongozo wa maisha yetu, sasa inaonyeshwa kwa wanadamu kama kipimo kinachotumika katika hukumu. Ule mkono unazifungua mbao zile, kisha zinaonekana kanuni za Amri Kumi, zikiwa zimeandikwa kama kwa kalamu ya moto. Maneno yale yako wazi kiasi kwamba watu wote wanaweza kuyasoma. Kumbukumbu inaamshwa, giza la upotofu na uzushi linafagiliwa kutoka katika akili ya kila mtu, na maneno yale kumi ya Mungu, mafupi, yanayoeleweka, na yenye mamlaka, yanaonyeshwa kwa wakazi wote wa dunia.

“Haiwezekani kuieleza hofu kuu na kukosa tumaini kutakakowapata wale waliozikanyaga amri takatifu za Mungu. Bwana aliwapa sheria yake; wangepaswa wawe wamelinganisha tabia zao na sheria hiyo na kuzijua kasoro zao wakati ule ilipokuwapo bado nafasi ya kutubu na kufanya matengenezo; lakini ili kujipatia kupendwa na ulimwengu, waliziweka kando amri zile na kuwafundisha wengine kuzikiuka. Wamejitahidi sana kuwalazimisha watu wa Mungu kuidharau Sabato yake. Sasa wanahukumiwa na sheria ile ambayo wameidharau. Kwa utambuzi maalum wa kuogofya wanaona kwamba hawana udhuru....

“Wakiwa wamechelewa wanaiona tabia halisi ya sabato yao ya uongo na msingi wa mchanga mahali ambapo wamekuwa wakijenga. Wanagundua kwamba wamekuwa wakipigana dhidi ya Mungu. Walimu wa kidini wameongoza watu kwenda kwenye uharibifu huku wakidai kuwaongoza kwenda katika malango ya Paradiso.” — *The Great Controversy*, pp.639,640.

## 5. SURA YA MWISHO — Alh, **Mar 26**

a. Eleza hatima ya mwisho ya watenda maovu. Malaki 4:1–3.

b. Je, ni wito gani wa mwisho ambao Mungu anatuma kutoka kwa manabii wadogo? Malaki 4:5, 6 .

Ni hali ya kidunia na ubinafsi ndivyo hutengana na Mungu. Ujumbe kutoka mbinguni una tabia ya kuamsha upinzani. Mashahidi waaminifu wa Kristo na Ukweli watakemea dhambi. Maneno yao yatakuwa kama nyundo ya kuvunja moyo wa gumegume, kama moto uteketezao taka. Kila wakati kuna haja ya kutolewa ujumbe wa dhati, na mahususi wa onyo. Mungu atakuwa na watu ambao ni waaminifu kwenye wajibu wao. Kwa wakati unaofaa Yeye hutuma wajumbe Wake waaminifu kufanya kazi sawa na ile ya Eliya." — *Testimonies for the Church*, vol.5, p.254.

"Sio mpaka wazazi wenyewe watembee katika sheria ya Bwana kwa mioyo mikamilifu ndipo watakapokuwa tayari kuwaamuru watoto wao baada yao. Matengenezo katika suala hili yanahitajika—matengenezo ambayo yatakuwa ya kina na mapana. Wazazi wanahitaji kurekebisha; wachungaji wanatakiwa kufanya matengenezo; wanamhitaji Mungu katika nyumba zao.Ikiwa wangeona hali tofauti ya mambo, lazima walete neno Lake katika familia zao na lazima walifanye kuwa mshauri wao. Ni lazima wawafundishe watoto wao kwamba ni sauti ya Mungu inayoelekezwa kwao, na inapaswa kutiiwa kikamilifu.Wanapaswa kuwafundisha watoto wao kwa subira, na kuwafundisha kwa fadhili na bila kuchoka jinsi ya kuishi ili kumpendeza Mungu. Watoto wa kaya kama hiyo wamejitayarisha kukutana na hali ya ukafiri.Wamekubali Biblia kuwa msingi wa imani yao, na wana msingi ambao hauwezi kufagiliwa mbali na wimbi linalokuja la mashaka." — *Patriarchs and Prophets*, p. 143.

"Familia ya Kikristo yenye mpangilio mzuri ni hoja yenye nguvu inayounga mkono ukweli wa dini ya Kikristo—hoja ambayo kafiri hawezi kuipinga....Ikiwa nyumba za wanaodai kuwa Wakristo zingekuwa na utii unaofaa wa kidini, zingetoa ushawishi mkubwa kwa ajili ya wema. Kwa kweli zingekuwa 'nuru ya ulimwengu.'" — *Ibid.*, p. 144.

## MASWALI TAFAKARI BINAFSI — Ijum, **Mar 27**

1. Iwe nimeoa au la, ninawezaje kuimarisha mpango wa Mungu wa ndoa?
2. Ni kwa njia gani ninaona ushahidi wa mchakato wa utakaso wa Mungu ndani yangu?
3. Taja vitabu vitatu vya kumbukumbu vilivyotajwa katika mahakama za Mbinguni.
4. Ninawezaje kuleta furaha kwa moyo wa akili za mbinguni?
5. Ni mahubiri gani yenye nguvu zaidi ambayo yameitishwa katika siku hizi za mwisho?

# Sadaka za Sabato ya Kwanza



## Sabato, 3 Januari, 2026

**Makao makuu huko Siguatepeque, Honduras**

Sasa ni nafasi yetu ya kusaidia kutengeneza nafasi kwa ofisi zinazohitajika haraka, vyumba vya mikutano, na madarasa ya shule ya wamisionari (Tazama uk. 4).



## Sabato, 7 Februari, 2026

**Idara ya Ustawi wa GC**

Maafa yanaongezeka kila mahali. Bwana anamwita kila mmoja wetu kufanya kile anachoweza ili kusaidia kupunguza maumivu na mateso! (Tazama uk. 30).



## Sabato, 7 Marchi, 2026

**Field ya Maranhão Piauí (AMAPI) Makao Makuu, Brazili**

Ofisi za utawala, malazi, na ukumbi vinahitajika ili kuendeleza field hii inayokuwa. Hebu tusaidie kuifanya! (Tazama uk. 51).